FORM THREE HOLIDAYS SMART PASS

KISWAHILI PP2 10 QUESTION PAPERS



FORM 3 HOLIDAYS SMART PASS

KISWAHILI PP2

TEN QUESTION PAPERS

Prefer Calling Amobi Group of Examiners

@ 0743 333 000 OR 0706 851 439

For Marking Schemes

N/B In Response to the Huge Costs Associated in Coming Up with Such/Similar Resources Regularly, We inform us All, MARKING SCHEMES ARE NOT FREE OF CHARGE. However Similar QUESTIONS, Inform of soft Copies, are Absolutely FREE to Anybody/Everybody. Hence NOT FOR SALE

by Amobi Group of Examiners.


CALL AMOBI GROUP OF EXAMINERS @ 0743 333 000 OR 0706 851 439 TO ACQUIRE :













FORM THREE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI PP2 KAATASI NAMBARI: 01

1. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Habari kuwa watoto chini ya miaka mitatu ‘huwindwa’ kitandani na kuraushwa na wazazi wao waende shuleni mwendo wa saa kumi na moja asubuhi ni za kusikitisha.

Kwa mujibu wa ripoti za wataalamu wa elimu ya watoto wachanga (ECD), watoto hao hutakikana kuwa darasani kabla ya saa kumi na mbili asubuhi.

Wanapowasili wao huanza kufukuza ratiba ya masomo ambayo huwapatia muda mfupi mno wa kula, kucheza, kupumzika na hata kuchunguza afya na usalama wao.

Badala ya kuondoka mapema kuelekea nyumbani, wengi wao hufika saa za usiku pamoja na wazazi wao wakitoka kazini. Wanapowasili nyumbani wanapaswa kuoga na kupata chakula cha jioni kwa pupa ili wafanye mazoezi waliyopewa na walimu wao.

Mazoezi hayo huwa ya masomo yote matano huku kila somo likiwa na zaidi ya maswali thelathini.

Badala ya kupumzika mwishoni mwa juma, watoto hao huhitjika kuhudhuria shule siku nzima ya Jumamosi. Jumapili wanatakiwa Kanisani na hali hii hujirudia mpaka muhula umalizike. Ikiwa ulidhani watapewa nafasi ya kupumzika wakati wa likizo , umekosea kwa sababu watoto hao huhitajika kuhudhuria shule. Hili limekuwa likiendelea hata baada ya Wizara ya Elimu kupiga marufuku kusomesha wakati wa likizo.

Wazazi-hasa wale wanaofanya kazi mijini- wamekuwa wakiunga mkono mtindo huu kwa sababu unawaondolea mzigo wa malezi na gharama ya kuwaajiri walezi.

Wataalamu wanasema matokeo ya hali hii ni watoto **wakembe** wenye afya na **maadili** mabaya kutokana na kuchanganyishwa akili na walimu wanaowataka wajue kila kitu wakiwa na umri mdogo.

Kuwashinikiza watoto wakembe wahudhurie shule na zaidi ya hayo wajue kila kitu kuna madhara mengi. Kwanza kabisa, kuraushwa kwa watoto macheo waende shule kunawanyima fursa ya kulala na kupumzika. Utafiti unaonyesha kuwa watoto wanahitaji kulala na kupumzika kwa zaidi ya saa 12 kwa siku. Hii ina maana kuwa mbali na muda mfupi wanaolala na kupumzika mchana kutwa, watoto wanapaswa kutumia usiku mzima kwa usingizi.

Hii huwasaidia kukua wakiwa na afya nzuri hasa kiakili. Matokeo ya kuwarausha watoto hao waende shule saa hizo huwafanya wakose furaha mbali na kuwafanya wachanganyikiwe kiakili.

Pili, kuwalazimisha watoto wakae darasani kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni huwa kunawanyima fursa ya kucheza na kutangamana. Wataalamu wa afya ya watoto wanapendekeza kuwa watoto wachanga wanapaswa kucheza ili viungo vya miili yao kama moyo, akili, mapafu na kadhalika vifanye kazi vizuri.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Kinyume na watu wazima ambao hufanya kazi nzito nzito na kuwawezesha kufanya mazoezi, watoto huwa hawafanyi kazi hizo. Wazazi na walimu wanapaswa kufahamu kuwa kazi ya watoto ni mchezo na wana kila haki ya kupewa furaha ya kucheza wakiwa shuleni na hata nyumbani.

Tatu, wazazi wengi ambao hufurahia kuwaachia walimu jukumu la kuwalea watoto wao huku wao wakiwa kazini huwa wanasahau kuwa sio kila mwalimu ana maadili yanayopaswa kuigwa na mwanawe. Ingawa tunawatarajia walimu wawe mifano bora ambayo inaweza kuigwa na kila mtu, ukweli ni kwamba baadhi ya walimu hawajui maana wala hawana maadili. Hatari ni kwamba watoto **wakembe** husoma kwa kuiga wakubwa wao na ikiwa walimu wanaoshinda nao shule wamepotoka kimaadili, kuna uwezekano mkubwa wa watoto hao kupotoka pia. Hii ndiyo sababu wazazi wengi wamekuwa wakilalamika kuwa wanawao tabia mbaya ambazo hawaelewi zilipotoka.

Kila mzazi anayejali maisha ya mwanawe anapaswa kutekeleza jukumu lake la kumlea na kumwelekeza jinsi anavyotaka akue. Ni kinaya kuwa wanawatarajia wanawao wawe na tabia na maadili kama yao ilhali hawachukui muda wa kukaa nao na kuwaelekeza.

Nne, kuwawinda, kuwaamsha, kuwaosha na kuwalazimisha watoto waende shule kila siku hata ingawa hawataki huwa kunawafanya wawe wategemezi wasioweza kujipangia na kutekeleza mambo kivyao.

MASWALI.

(a) Ipe taarifa anwani mwafaka. **(ala2)**

(b) Mwandishi anatoa maoni gani kuhusu ratiba ya masomo? **(alm2)**

(c) Eleza athari za mfumo wa elimu unaoangaziwa hapa. **(alm3)**

(d) Ni ushauri upi unaotolewa kwa wazazi ? **(alm2)**

(e) Taja mbinu zozote **mbili** za lugha alizotumia mwandishi **(alm2)**

(f) Eleza **maana** ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa. **(alm4)**

(i) **'huwindwa' kitandani**

(ii) **Maadili**

(iii) **Kuwashinikiza**…

(iv) **Wakembe**…

1. Soma taarifa kisha fupisha kwa mujibu wa maswali yafuatayo.

Uwezo wa kuyakumbuka mambo ni hazina kuu kutoka kwa mtu yeyote yule aliye hai. Uwezo huu wa kukumbuka ni mojawapo ya shughuli changamano za ubongo. Ubongo wa mwanadamu hutekeleza shughuli hii kwa namna tatu. Kwanza ubongo hunasa jambo kisha huliihifadhi. Baadaye huanzisha mfumo wa kutoa kilicho hifadhiwa. Ubongo ukiathirika kwa namna yeyote katika moja wapo ya njia hizi, basi uwezo wa kuyakumbuka mambo huvurugika.

Ingawa inaaminika kuwa uwezo wa kukumbuka hurithishwa toka kizazi kimoja hadi kingine,

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

wataalamu wa maswala ya kiakili wanabaini kuwa uwezo huu unaweza kuimarishwa. Uimarishaji huu huhitajika mikakati madhubuti.

Njia mojawapo ya kustawisha uwezo wa kukumbuka ni kupitia kwa lishe. Vyakula vilivyosheheni vitamini B vyenye amino asidi husaidia kuimarisha uwezo wa kukumbuka. Vyakula kama hivi ni mboga, nyama (hasa maini), bidhaaa za soya, matunda, maziwa, ,bidhaa za ngano, samaki, pamoja na mayai. Vyakula vingine muhimu katika ustawishaji huu ni vile vyenye madini ya chuma. Madini haya huwezesha usambazaji wa hewa katika ubongo kwa wepesi. Vyakula ambavyo vina madina haya ni mboga za kijani, mawele, ndengu, soya, matunda kama maembe, ufuta (simsim) pamoja na nyama, hasa maini na mayai.

Ubongo wa mwanadamu aliye hai hufanya kazi kila wakati awe macho au amelala. Utendaji kazi wake huendeshwa na glukosi mwilini. Kwa hivyo, vyakula vyenye sukari hii ni muhimu kuliwa. Hata hivyo, lazima mtu awe mwangalifu na kuhakikisha kuwa mwili una kiwango cha sukari kisicho hatarisha maisha. Haya yanawezekana kwa kula vyakula vyenye nyuzinyuzi kama vile mboga na matunda.

Njia ya pili ni kupiga marufuku vileo kama pombe na nikotini. Vileo hivi huathiri utaratibu wa kunasa, kuhifadhi na kutoa yaliyo ubongoni.

Iwapo mtu ana tatizo la kuyakumbuka majina ya watu, ni muhimu kufanya mazoezi ya kusikiliza kisha kurudia majina hayo wakati wa mazungumzo. Ni bora kulihusisha jina na sura ya mtu. Kwa njia hii ubongo utanasa jina na kile kinacholengwa.

Woga na kuvurugika kiakili ni mambo mengine tunayopaswa kuepuka kila wakati. Ni kawaida mtu kupata woga wakati anapokabili jambo asilokuwa na uhakika na matokeo yake kama mtihani au mahojiano. Lakini anapaswa kuwa makini. Woga huo usikiuke mpaka na kumvuruga kiakili. Vurugu hizi huathiri kilichohifadhiwa ubongoni na pia namna ya kukitoa.

Halikadhalika, mwili wenye siha nzuri huhakikisha kuwa ubongo ni timamu. Wataalamu wengi wa siha wanakubali kuwa na mazoezi ya kunyoosha viungo hustawisha ubongo na hivyo kuhakikisha kuweko kwa uwezo wa kukumbuka mambo. Ni muhimu kuwa na taratibu ya kunyoosha viungo kila wakati. Fauka ya hayo, mazoezi ya kiakili, kama vile kusoma makala yanayovutia, kujaza mraba na michezo mingine kama mafumbo, vitenzi ndimi ni muhimu katika kustawisha uwezo wa kukumbuka.

Jamii ya watu wenye uwezo kuyakumbuka mambo ni ya jamii iliyopiga hatua kimaendeleo. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuimarisha uwezo wa kukumbuka kila wakati.

Maswali:

a) Kwa maneno 60 – 65 fupisha mchango wa chakula katika uimarishaji wa uwezo wa kukumbuka.(alama 6 ,2 mtililiko)

b) Fupisha aya tatu za mwisho kwa maneno 80 – 90 **(alm7)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

3. MATUMIZI YA LUGHA

. (a) Andika sifa bainifu za sauti. **(alm2)**

(i) e:-

(ii) n:- .

(b) Eleza maana ya :- **(alm2)**

(i) Kiimbo.

(ii) Shadda.

(c) Tunga sentensi moja moja kudhihirisha ngeli zifuatazo:- **(alm2)**

(i) U-U

(ii) Pokomo /Pa-ku-mu

(d) Unda kitenzi kimoja kutokana na nomino '**Mtubia**" **(alm2)**

(c) Eleza matumizi mawili ya kiambishi '**ku**' **(alm2)**

(f) Tunga sentensi ya maneno manne ambayo ina sehemu zifuatazo. Kielezi cha namna, kivumishi,kitenzi na jina **(alm2)**

(g) Yakinisha sentensi ifuatayo; **(alm2)**

Mvua haijanyesha vizuri msimu huu.

(h) Onyesha matumizi mawili mawili ya alama zifuatazo:- **(alm2)**

(a) Alama ya mshangao

(b) Mshazari

(i) Tunga sentensi sahihi ukitumia –wa- katika kauli ya kutendeana **(alm2)**

(j) Andika udogo wa sentensi:- **(alm2)**

Ndama wa ng'ombe yule ameuzwa.

(k) Onyesha tofauti ya vitate vifuatavyo kwakuvitungia sentensi **(alm2)**

(i) Dhamani

(ii) Thamani

(l) **Kanusha sentensi ifuatayo katika wingi** **(alm2)**

Ningalikuwa na pesa ningalinunua gari

[m] Tumia neno "shujaa" katika sentensi kama:- **(alm2)**

(i) Kivumishi

(ii) Kielezi.

(n) Huku ukitumia mifano mwafaka, eleza tofauti ya sentensi sahili na ambatano **(alm4)**

(o) Onyesha aina za viambishi katika sentensi hii: **(alm2)**

Nitajisomea

(p) Andika katika usemi wa taarifa:- **(alm2)**

Tutaanza mashindano kesho, Mwalimu alimwambia mwanafunzi.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

(q) Eleza maana mbili ya sentensi:- **(alm2)**

Tumetengeneza barabara

(r) Tumia mifano mwafaka kueleza aina za mofimu **(alm2)**

(s) Changanua kwa njia ya mishale

Mama analima shambani.

4. ISIMU JAMII

Soma mzungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali *:*

A : Ohh, dada Naomi

B : Dada Ruth (anamsogea kwa bashasha wanakumbatiana). Ahh Mungu asifiwe!

A: Asifiwe sana

B: Ehh dadangu, miezi ...mingi...sijakuona

A: dada wee...Nilitumwa huko kusini ...Kuwahubiria watu injili (mtuo mdogo)singeweza kukata...

B: Ehh, usiwe kama Yona

A: Habari ya siku nyingi?

B; Nzuri Mungu bado ameendelea kunibariki

A: Amen!

B: Nimeendelea kuiona neema yake

A: Amen! Asifiwe Bwana

B: Halleluya

A: Ni Mungu wa miujiza!

B : Amen. Hata nami nimeona neema yake

Bado niko imara katika wokovu katika siku hizi za mwisho

A : Amen !

B : Ni Mungu wa ajabu kweli !

A : Nilikumbana na matatizo lakini nikategemea sala

Kama Paulo na sila… Na nikashinda (anatua). Sikuweza kumpa shetani nafasi…maana ameshindwa

B : Ameshindwa kabisa

<u>Maswali</u>:-

(i) Hii ni sajili ya wapi ? Fafanua **[alm2]**

(ii) Taja na ueleze sifa za sajili hii **[alm6]**

(iii) Taja mambo **mawili** muhimu yaliyosaidia katika maenezi ya Kiswahili Afrika mashariki na kati. **[Alm2]**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM THREE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI PP2 KARATASI NAMBARI: 02

1. UFAHAMU (Alama 15)

Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali

Huku ulimwengu unapoingia katika teknologia ya tarakilishi na sera ya utandaridhi, ukweli wa mambo ni kuwa akina mama wamezinduka. Suala la usawa wa kijinsia limeanza kushamiri kote duniani na ole wake mwanamume yeyote ambaye hajawa tayari kutembea na majira. Lakini hebu tuchunguze jambo hili kwa makini zaidi.

Usawa wa jinsia ni nini? Usawa wa kijinsia ni usawa wa binadamu wote; wawe wake au waume. Usawa huu unapaswa kudhihirika katika kugawa nafasi za kazi, utoaji wa elimu, nafasi za uongozi na nyanja nyinginezo zozote za maisha.

Ubaguzi wa aina yoyote ile hasa dhidi ya mwanamke ni jambo linalokabiliwa na vita vikali sana ulimwenguni kote.

Dahari na dahari, hasa katika jamii za kiafrika, kumekuwa na imani isiyotingisika kuwa mwanamke ni kiumbe duni akilinganishwa na mwanaume. Kwa hivyo mwanamke amekuwa akifanyiwa kila aina ya dhuluma ikiwepo kupigwa, kutukanwa, kudharauliwa, kunyimwa haki zake, kunyimwa heshima na mambo kama hayo. Lakini je, ni kweli kuwa mwanamke ni kiumbe duni asiyefaa kutendewa haki?

Tukichunguza jamii kwa makini tunaweza kuona mara moja kuwa hivyo ni imani potofu isiyo na mashiko yoyote. Ukiimulika familia yoyote ile iliyopiga hatua kimaendeleo, uwezekano mkubwa ni kuwa mume na mke wa familia inayohusika wana ushirikiano mkubwa. Mume anamthamini mke wake na hadiriki kufanya maamuzi muhimu yanayoweza kuathiri maendeleo ya familia bila kumhusisha mke. Mume kama huyo huketi na mkewe, wakishauriana na kufikia uamuzi bora.

Tukitoka katika muktadha wa kifamilia na kumulika ulimwengu wa kazi iwe ni katika afisi za kiserikali au kwenye makampuni binafsi, ukweli ni kwamba kiongozi yeyote yule aliyefaulu katika usimamizi wake mara nyingi huwa na mke nyumbani ambaye wanashauriana kila uchao kuhusu kazi anayofanya hata kama mke hafanyi kazi mahali pale. Hisia na mawaidha anayotoa mke kwa mume wake ni tunu na huenda asiyapate kwingineko kokote hata katika vitabu vya kupigiwa mifano. Hii ni mojawapo ya sababu ambayo huwafanya viongozi wa nchi mbalimbali kupenda sana kuwatambulisha wake na familia zao waziwazi kwa vile wanajua kuwa jamii inathamini sana msingi wa jamii. Kiongozi ambaye hana mke au familia au yule ambaye mke wake hatambuliki, hutiwa mashaka na jamii hata kama ni kiongozi aliye na azma ya kushikilia kazi ngumu ya kuongoza umma.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Tukirudi nyuma kidogo na kupiga darubini mataifa ya mbali, tunaweza kuwaona wanawake mashuhuri walio uongozini ambao hadi waleo unapigiwa mfano. Wanawake mashuhuri waliotoa uongozini ambao hadi waleo unapigiwa mfano. Wanawake hao walisimamia mojawapo ya mataifa yenye uwezo na ushawishi mkubwa zaidi duniani. Ingawa wengi wao sasa wameng'atuka, uongozi wao bado unakumbukwa hata baada ya miaka mingi ya wao kuamua kupumzika, Mifano ni kama: Bi Margaret Thatcher aliyekuwa waziri mkuu wa Uingereza, Bi Bandranaike wa Sri Lanka, Golda Meir wa Israel na wengine wengi katika mataifa kama Indonesia, Ufilipino, Bangladesh, Pakistani na kwingineko.

Katika kufikia tamati, tunapozungumza kuhusu jinsia, hatuna budi kugusia kitafsili masuala nyeti. Kwanza, imani ya kushikilia kikiki tamaduni zisizofaa, ni jambo linalofaa kuchunguzwa kw makini. Kwa mfano, kuna badhi ya jamii ambazo humlazimu mke kurithiwa baada ya kifo cha mumewe. Vile vile baadhi ya jamii za kiafrika zinashikilia kuwa mwanamke hana haki ya kurithi. Kutokana na imani hii, wanawake wengi huishi maisha ya taabu baada ya kutengana na waume zao kwa vile hawana haki ya kurithi chochote kutoka kwa wazazi wao hata kama wazazi hao wana mali nyingi kupindikukia. Mali ya wazazi ni haki ya watoto wa kiume wala si watoto wa kike! Hili ni jambo la kusikitisha mno.

Isitoshe, wanawake hukumbwa na kizingiti kingine wanapojaribu kumiliki mali ya waume zao baada ya waume hao kukata kamba. Sababu ni kuwa, baada ya hao wenda zao kuwekwa kaburini, vita vya umiliki wa mali huanza mara moja na mwishowe yule mke maskini hujikuta hana hata mahali pa kulala sembuse mali waliyochuma na mali yake yote kunyakuliwa na aila ya mumewe . Jambo hili linaonyesha namna tulivyoachwa nyuma na uhalisia wa mambo. Ni lazima jamii izinduke na itoke kwenye kiza hiki chenye maki nzito.

MASWALI

(a) Ina maana gani kusema kuwa wanaume hawana budi "kutembea na majira?" **(alm2)**

(b) Kabla ya uzinduzi huu kuhusu usawa wa kijinsia, wanawake wamekuwa wakitendewa dhuluma za kila aina. Taja tatu. **(alm3)**

(c) Je, ni kwa nini viongozi wengi hupenda kujitambulisha na familia zao? **(alm2)**

(d) Je, unaamini kuwa hisia na mawaidha anayotoa mke kwa mume wake ni tunu na huenda yasipatikane kwingineko? Fafanua **(alm2)**

(e) Je licha ya kunyimwa haki yake ya kujiamulia, ni matatizo yapi mengine yanayoweza kumukumba mke anayelazimishwa kurithiwa? **(alm3)**

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumiwa katika muktadha. (alama 3)

Kushamiri

Hulka

Azma

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

MUKHTASARI (Alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali yatakayofuata.

Binadamu hupenda kujivika vilemba vingi mno.Tunapenda kuheshimiwa na kutukuzwa na kila mtu. Tunapenda kuombwa ushauri na wote ambao wanahitaji ushauri! Tunapenda kutambuliwa popote tuendapo.

Watu wengi hukataa kufanya jambo la halali kwa kuhofia kuitwa wajinga. Mfano mzuri ni pale ambapo mtu amekosea kidogo katika kutenda jambo; utaona kuwa mtu huyo anaona ugumu wa kuomba radhi au samahani ati kwa sababu ataonekana mjinga.

Je, ni mara ngapi mkurugenzi ameita mkutano na katika barua yake akatisha kuwaadhibu watakaochelewa na mwishowe ni yeye mwenyewe anayechelewa? Tena huwa haombi msamaha. Ataulaumu usingizi uliomchukua, au gari lililomleta.

Aghalabu tunapowakuza watoto wetu, tunawafunza maadili mema. Tunawahimiza wale wadogo kwamba ni vizuri kuomba radhi kwa wakubwa wako unapowakosea. Lakini kumbuka kwamba kukosea ni kwa binadamu wote. Mtu anaweza kukukosea kwa makusudi au kwa bahati mbaya. Kwa hivyo tunapaswa kufahamu kwamba, tunapofanya makosa ni lazima tuombe msamaha, iwe ni kwa wakubwa au kwa wadogo, ili kuondoa kero.

Waja wengi huogopa kusimama mbele za watu na kuwasilisha au kutenda jambo fulani. Kisa na maana, mtu hataki kutenda jambo fulani halafu akosee. Hajiamini na anaogopa kuwa huenda watu wakaona kasoro yake. Lakini kumbuka, kukosa njia ndiko kuijua.

Huenda ikawa watu wanajadili maswala ibuka kama vile ufisadi, kuavya mimba, matumizi ya dawa za kulevya, ukimwi, uzuiaji wa kizazi na kadhalika... labda huyaungi mkono maoni ya watu wengine kwa sababu ya imani na maadili yako. Hata hivyo, hutaki kusimama ukatoa msimamo wako mbele za watu ingawa dhamiri yako imekwazika. Baadaye utasikika ukiwalaumu watu wengine ilhali ulikataa kusimama na kutetea msimamo wako.

Wengi wetu hujichukua kuwa watu muhimu sana. Wanaona kuwa sherehe au mkutano wowote hauwezi kufaulu ikiwa wao hawako. Wanapokuwa kwenye hiyo mikutano wao hutaka watambuliwe. Hupenda majina yao yatajwe. Haya huwaridhisha , lakini swali ni je, kuwepo kwao ni muhimu kiasi hicho? Kumbuka kwamba mkutano ungeendelea vizuri bila kuwepo kwao. Kwa hivyo, tusiwe watu wa kutaka kutambuliwa kila tunapoenda mahali. Pia, tusilalamike ikiwa hatukuhusishwa katika jambo fulani.

Unaposhuhudia jambo fulani, kama wizi au ajali, usiwe na woga wa kutoa usaidizi kwa kutoa ushuhuda. Wengine hata huogopa kutoa usaidizi huo, hata kwa manusura wa ajali za barabarani, eti kwa sababu wanahofia kuitwa mahakamani kutoa ushuhuda. Kuna shida gani kuenda kusema yale uliyoyashuhudia bila kuongeza au kutoa chochote?

MASWALI

a) Bila kupoteza maana, fupisha aya ya kwanza hadi ya nne.(maneno 60) **(alm7)**

b) Fupisha aya nne za mwisho. (maneno 50) **(alm8)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

a. Taja tofauti iliyopo kati ya sauti /f/ na /v/ **(alm1)**

b. Andika sentensi ifuatayo ukitumia kinyume cha neno lililoandikwa kwa herufi ya mlazo: **(alm1)**

Binadamu hawezi *kumuumba* mwenzake.

c. Andika sentensi ifuatayo upya ukizingatia kisawe cha neno lililopigwa mstari: **(alm1)**

Mtoto mwenye <u>hamaki</u> hawezi kuelewa maagizo.

d. Andika kwa usemi halisi: **(alm3)**

Yule mshukiwa aliyekamatwa na polisi alisema kuwa papo hapo ndipo alipoficha ule mkufu.

e. Tunga sentensi inayoshirikisha nomino uliyopewa pamoja na vipashio vifuatavyo vya sarufi: kivumishi kisisitizi, kitenzi kishirikishi, kitenzi, na kielezi cha wakati. **(alm2)**

Pinde……

f. Sahihisha sentensi zifuatazo :

(i) Ndegwa alipeana kalamu yake kwa mwanafunzi. **(alm 1)**

(ii) Siku hizi mahitaji imezidi na pesa haitoshi. **(alm 1)**

g. Tunga sentensi mbili kubainisha maana mbili tofauti za neno: **rudi.** **(alm2)**

h. Akifisha: **(alm2)**

Mtume asimame nusura aingie kwenye shimo la taka

i. Unda nomino kutokana na kivumishi:**refu** **(alm1)**

j.Onyesha chagizo katika sentensi ifuatayo: **(alm1)**

Watu wanne walipeperushwa juu kwa juu na upepo mkali.

k. Tunga sentensi ukitumia**: isije ikawa** **(alm2)**

l. Andika upya sentensi ifuatayo ukitumia virejeshi vya tamati: **(alm2)**

Mwanafunzi anayefanikiwa maishani ni yule anayesoma kwa bidii na pia anayewatii wazazi wake.

m. Ainisha viambishi awali na tamati katika sentensi: **Anikumbukaye** **(alm2)**

n. Kanusha kwa udogo: Mwizi aliiba kikapu na ng'ombe. **(alm2)**

o. Andika umoja wa sentensi: **(alm1)**

Kwato za wanyama hutufaidi.

p. Andika kwa wingi : **(alm4)**

Wimbi hilo la maji lilimhofisha mvuvi akashindwa kutupa wavu wake majini.

q. Andika katika hali ya kutendewa: **(alm2)**

Kuku hawa wamemsumbua Sabina kwa muda mrefu.

r. Tumia sentensi moja moja kubainisha tofauti kati ya sentensi **sahili** na sentensi **ambatano (alm2)**

s.Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mistari au mishale:

Mwanasiasa aliyewapuuza wanaeneo bunge lake amekomelewa. **(alm4)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

t. Andika katika usemi wa taarifa. **(Alm2)**

"Karibu Bakari, tafadhali kaa", Maimuna alisema. "Asante, je, habari za nyumbani?" Bakari aliuliza.

u. Taja aina ya yambwa iliyopigiwa mstari katika sentensi uliyopewa: **(alm1)**

Mpishi amempikia <u>mgeni</u> wali vizuri.

ISIMUJAMII (Alama 10)

(a) Taja nadharia zozote mbili zinazohusiana na chimbuko la lugha ya Kiswahili. **(alm2)**

(b) Kwa kutolea mifano, eleza sifa zozote nne za kimsingi za sajili inayoweza kutumika darasani. **(alm8)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM THREE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI PP2 KARATASI NAMBARI: 03

UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Siku moja , mtu ambaye alijulikana kwa jina la Moto, alikuwa ameketi chini ya kivuli cha mbuyu. Alikuwa akifanya hivyo kwa kungojea kulungu kunaswa na mtego wake. Hapo mbuyuni, ndipo palikuwa na njia ya kulungu ya kwenda mtoni kunywa maji. Kupitia mbuyuni, iliwabidi kwanza wapitie pale mtegoni. Lakini kwa kuwa kwa siku hii ya leo wakati wao wa kunywa maji ulikuwa bado kuwadia, naye Moto, badala ya kurudi ili aje baadaye, akaonelea heri angojee hapo.

Haikuwa mara yake ya kwanza kutega kulungu. Alikuwa amewanasa wengi na kwa muda mrefu sana. Na ingawaje alifurahia nyama yao laini, ni kuwachuna ndiko alikokuzira. Hii ilikuwa ni kwa sababu ya vifaa butu vya mawe ya kuchonga alivyokuwa akitumia. Kwa sababu hii basi, haikuwa rahisi kuwachuna. Pia, alikuwa akiwala wabichi. Ili kujipa kazi akisubiri, akaonelea amtengenezee utunda mpenzi mkewe. Hakuwa na shida kuamua utunda huo ungekuwa wa namna gani. Nyakati hizo, shanga zilikuwa bado hazijavumbuliwa. Ni jiwe na mti tu ndivyo vilivyokuwapo, navyo ndivyo vilivyokuwa mali ghafi.

Kwa ala yake, jiwe la kuchonga, Moto akakata vijiti viwili. Kikubwa akakiita 'mama' na kidogo, 'baba'. Dhamira yake ilikuwa kumtengenezea mkewe ushanga na tembe zikiwa za mti. Akiweka kijiti mama chini, alitumia kijiti baba kupekejea tundu. Alifanya hivi kwa nguvu zake zote, Haja ilikuwa ni atoboe matundu mengi, halafu ayakate na kuyaviringisha na baadaye ayaunge na uzi wa mua ili apate huo ushanga. Akizidi kupekecha, na jasho kumtoka, na huku mawazo yake yote yakiwa juu ya uso wa mkewe, hakuwa ameona cheche zikianguka juu ya majani makavu yaliyokuwa katikati ya mapaja yake. Alichokisikia kwa ghafla, kilikuwa ni kuchomeka na kuona moshi ukifusika. Alishtuka na akaruka kwa woga. Hakuwa ameshawahi kuona kioja kama hiki maishani!

Huku akitetemeka kwa hofu, cheche hiyo ikaanza kusambaa. Ilijieneza kwa haraka na kuwasha majani, nyasi na miti. Sasa ikawa imepata nguvu na kuenea kwa upesi na kumeza vichaka na misitu iliyokuwa mbele yake. Kuangalia hivi, akajiona amesimama peupe! Kutoka kwa upande wa mtegoni, kukaja harufu nzuri ya kunukia. Alifuata na alipofika, akaona kulungu ambaye alikuwa ameshikwa na mtego, ameokwa vizuri sana na nguvu hizo ngeni. Hakujua zinaitwaje wala hakujua aziiteje. Kwa hivyo, hakuwa ameshawahi kuona ama kuonja kitu cha kuchoma sembuse cha kupikwa!

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Ni harufu ya kuiva ya kulungu na kudondoka kwa mafuta ya kunona ndivyo vilimtia ujasiri. Naye kwa hatua za woga, akanyatanyata akanyakua kinofu na kukionja. Si utamu huo aliousikia! Sasa akanyafua jinofu. Halafu akaingilia maini, moyo na mafigo. Kulungu akamshinda ingawaje alimla maradufu ya kawaida yake. Aliyebaki, akamfunga ndani ya majani ya mgomba na kuwapelekea watu wake. Pamoja na kulungu, akawa amechukua pia kinga kilichokuwa kikiwaka na vile vijiti viwili ambavyo baadaye kijiti mama alikuja kukiita "wimbombo" na kijiti baba, " ulindi"...

Ilikuwa alfajiri asubuhi watu waliposhtukia "tatata" za kualika kwa kuni na kulipuka kwa moshi kutoka nyumbani kwa Moto. Nyumba yenyewe ilionekana ikiwa na nuru nyekundu ya ajabu na ya kutisha. Walinyatanyata kuelekea kwenye kioja hicho. Kiliwavutia zaidi kwani walivyozidi kulisongelea, ndivyo ile baridi ya asubuhi ilivyozidi kuwatoka. Mvuto huo ukawapumbaza. Lakini walipumbazika zaidi walipoona - nyuma ya kioja hicho na kupita pazia la moshi, Moto ameketi.

Macho yake yalionekana mekundu mno. Hii ilikuwa sababu ya moshi; lakini hawakuwa wakijua hivyo. Kiwiliwili chake kilionekana kikiyumbayumba nyuma ya miale. Haya yote yakamfanya kutisha. Wenzake wasijue la kufanya kwa sababu ya bambuazi, wakawa wamesimama tuli wameduwaa. Hapo ndipo waliposikia sauti ikinena: "Mimi ndimo Moootoo...; naivisha na kuunguza, natokeza na naoteka. Anitakaye nitakuja kwake nimpe huu uwezo wangu..."

Ili kuwaogofya zaidi, akaupulizia nao ukaalika kwa moshi na cheche nyingi zilizowafanya wenzake kurudi nyuma kwa hofu. Kuona hivi, akaendelea kuwatia woga kwa kusema, "Hizi ndizo nguvu za Moootoo... mimi ndimi Moootoo...nijieni niwageuzie maisha yenu..."

Akiwa bado ana sehemu ya nyama ya kulungu, akawagawia na kuwaambia wale. Kila mmoja wao akakubali kuwa ilikuwa tamu sana. Naye ndipo aliwaambia siri ya kioja. Hakuwaambia ule ukweli wa mambo, badala yake, aliwaambia ati ni malaika ndiye aliyemtunukia uwezo huo! Aliwalambisha kwa kuwapa kaa kuchukua makwao. Nao, kwa kukosa jina la kufaa, wakaliita "Moto".

Punde si punde, watu wakawa wamezoea moto na wengi wakawa wanakuja kwake tu. Hakutaka uenee vivi hivi tu. Kwa hivyo, akaweka masharti: moto ulipatikana kwake tu kila jioni, na uzimwe mara moja baada ya matumizi. Ni hapo kwake tu ambapo "moto mpya" ungeweza kupatikana. Moto hauibiki wala haufichiki, akawakanya. Na ambaye angefanya ujasiri wa kuuiba ama kuuficha, basi asije kulia kwake baadaye, akawaeleza.

Masharti haya yalifuatwa, naye akawa mgawaji wa moto wa pekee. Uwezo huu ulimtia hisia za ukubwa - na punde si punde, za utukufu pia! Sasa watu wakawa, bila moto, hakukuliwa kitu na basi kumtegemea yeye kukazidi. Hapa ndipo aliwageukia na kuwaambia:

“Ili kuulinda huu Moto Mtakatifu usife, imenibidi kuacha kazi zangu. Lakini siko radhi kuendelea kufa njaa na familia yangu."

" Tutakugawia chakula chetu ili uzidi kuuchunga huo Moto Mtakatifu ili usife," wakamkatiza.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Basi, kwa kila mtu kumpatia theluthi ya chakula chake, Moto akapata uwezo wa kurundika ziada. Siku si nyingi, mkewe na watoto wake wakawa hawana haja ya kufanya kazi. Hali watu hawakukoma kumpatia "kodi ya moto", ndivyo yeye na kizazi chake walivyozidi kujiepusha na kufanya kazi, huku wakizidi kuzua masharti magumu ya kuficha "Utukufu wa Moto".

Maswali

a) Ipe makala uliyosoma anwani mwafaka **(alm1)**

b) Moto alikuwa ameketi chini ya kivuli cha mbuyu kwa sababu gani? **(alm2)**

c) Eleza tabia zozote mbili za Moto kutokana na makala hii **(alm2)**

d) Taja na ueleze methali moja inayoweza kutumiwa kueleza matukio katika makala hii **(alm2)**

e) Taja masharti mawili yaliyowekwa na Bwana Moto kwa kutotaka Moto uenee hivi hivi tu. **(alm2)**

f) Moto na Aila yake walifaidikaje baada ya uvumbuzi huu? (alama 2)

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa. (alama 3)

(i) Kioja…

(ii) Alikokuzira……

(iii) wimbombo …

3. MATUMIZI YA LUGHA

(a)i)Taja ala zinazotumika katika kutamka sauti zifuatazo: **(alm2)**

(i) |dh|

(ii) |gh|

(b) Andika neno lenye muundo ufuatao **(alm1)**

irabu ya chini, nazali ya midomoni, irabu ya nyuma juu

(c) Bainisha miundo ya silabi katika maneno yafuatayo **(alm2)**

chura……

mbwa……

(d) Bainisha utendakazi wa viambishi katika neno lifuatalo. **(alm3)**

Kiliwaumiza

(e) Iiandike sentensi ifuatayo ukitumia kiwakilishi cha pekee o – ote. **(alm2)**

Ufunguo wowote ufunguao ni wetu.

(f) Eleza maana mbili za sentensi hii. **(alm2)**

Alitukimbilia kabisa.

(g) Andika katika kauli ya kutendesheka **(ala.2)**

(i) Iga

(ii) Vaa

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

(h) Andika udogo wa sentensi ifuatayo. **(ala.2)**

(i) Sahani zetu ni nzuri kuliko zao.

(i) Tumia ritifaa katika sentensi ili kuonyesha matumizi yake mawili **(alm2)**

(j) Andika katika wingi **(ala2)**

Kuku wa jirani kijijini mwetu aliangua kifaranga aliyelemaa.

(k) Tunga sentensi ukitumia nomino zifuatazo pamoja na kivumishi- ingine. **(ala 2)**

(i) Dau

(ii) Urembo

(l) Geuza katika usemi wa taarifa. **(ala.2)**

Karen: Tafadhali usiukanyage mguu wangu.

Chemosi: Ah! Mbona niukanyage?

(m) Tumia kielelezo cha jedwali kuchanganua sentensi.

Musa aligongwa na gari vibaya sana. **(ala.4)**

(n) Ainisha matumizi ya '-ema' katika sentensi ifuatayo. **(alm3)**

Mwanafunzi mwema ametuzwa vyema kwa wema wake.

(o) Yakinisha sentensi ifuatayo **(alm2)**

Uchaguzi mkuu hautafanyika mwaka huu

(p) Andika kulingana na maagizo yaliyotolewa. **(ala.2)**

Jina langu ni Omondi lakini huitwa Omosh kwa kifupi. (Anza kwa: Watu…….

(q) Onyesha virai vitatu katika sentensi hii na utaje ni vya aina gani. **(ala.3)**

Mtoto yule mdogo amekunywa maziwa kwa kikombe.

(r) Andika kinyume cha: **(ala.1)**

Walizama walipokuwa wakikusanya mchanga.

(s) Toa neno jingine lenye maana sawa na: **(ala.1)**

kariha

4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

Mhusika A : Wewe ndiwe Hatia Mpendamakosa? Kutokana na ushahidi uliotolewa, na kulingana na kifungu cha 55A cha sheria , ni wazi kuwa una mashtaka ya kujibu……

Mhusika B: (Akimkatiza kauli) Nakana Mheshimiwa!

Mhusika A: Mshatakiwa,jambo ulilofanya ni hatia kulingana na sheria za nchi. Ni hatia kwa mtu kuiba kitu hata kiwe kiasi gani. Sababu uliyotoa kwa kitendo chako pia haifai. Mahakama inakuhukumu kuihudumia jamii katika kifungo cha nje cha miezi sita. Kesi imekwisha.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Maswali:

(a) Lugha hii hutumika katika muktadha upi? **(ala.2)**

(b) Tambulisha wahusika **A** na **B** **(ala.2)**

Mhusika **A**:……

Mhusika **B**:……

e) Eleza sifa sita za sajili ya mazungumzo hayo. **(ala.6)**

FASIHI SIMULIZI (Alama 15)

Soma kifungu kufuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata

Mchuuzi wa mchuzi hana ujuzi wa mjusi wa juzi.

a. Tambua vipengele vifuatavyo vya kifungu hiki cha fasihi simulizi **(alm2)**

i) utanzu…

ii) kipera…

b. Kipera hiki kina sifa mbalimbali. Eleza zozote tano **(alm5)**

c. Kipera hiki kina umuhimu upi katika jamii yako? **(alm6)**

d) Andika mifano miwili zaidi ya kipera hiki **(alm2)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM THREE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI PP2 KARATASI NAMBARI: 04

1. UFAHAMU: (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia

Mateso ya wanawakiwa ni suala la kijamii linalofaa kutazamwa kwa darubini kali. Hata hivyo wanaoathirika zaidi ni watoto ambao bado wako katika umri unaohitaji kulelewa na kupewa mahitaji ya msingi kama mavazi, malazi, elimu na mengine anuwai. Hali ya kuachwa na wazazi imekuwa ikizikumba jamii tangu enzi za mababu na kila itokeapo, wanajamii huipokea kwa mitazamo tofautitofauti, hivyo kuwafanya wanawakiwa kuathirika sana.

Baadhi ya jamii zina imani za kijadi pamwe na mila zilizochakaa zinazozifanya kuamini kuwa baadhi ya vifo hutokana na laana. Wengine huchukulia kuwa mwendazake ameondolewa na ulozi. Imani kama hizi huifanya jamii kuwatia watoto walioachwa katika mkumbo ule ule, hivyo kuwaangalia kwa macho yasiyo ya kawaida. Hili husababisha dhana gande. Hali hii husababisha kuwachukulia watoto kama wanaotoka katika kizazi kilicholaaniwa. Jamii basi hukosa kuwapa watoto hawa stahiki yao. Hata wanapojitahidi kuiwania nafasi yao, waliowazunguka huwavunja mioyo. Jitihada zao huishia kuwa si chochote kwa kuwa jamii inawatazama kama waliolaaniwa.

Punde baada ya mzazi mmoja au wote wawili waendapo wasikorudi, inatarajiwa kwamba aliyeachiwa mtoto, awe mzazi wake, mwanafamilia au jirani awajibike na kumtunza mwanamkiwa. Kunao kadha wa kadha wanaowajibika – ninawavulia kofia. Hata hivyo wengi hutelekeza jukumu hili walilopewa na Muumba. Si ajabu basi kuona kuwa idadi ya watoto wanaozurura mitaani inazidi kuongezeka kila uchao. Ukichunguza utakuta kuwa wengi wa watoto hawa ni waliopotelewa na wazazi wao. Inakera zaidi kugundua kuwa baadhi ya watoto hawa wana mzazi mmoja. Kwamba mke au mume wa mtu ameaga, au iwe kwamba mzazi mmoja alimzaa mtoto na kumwachia mwenzake mzigo wa ulezi, aliyeachiwa ana jukumu la kumpa mwanawe mahitaji ya msingi. Machoni pa Jalali, kila anayeupuuza wajibu huu ana hukumu yake siku ya kiama!

Ni haki ya kila mtoto kupata elimu. Katika katiba ya Kenya mathalan, elimu ya msingi, yaani kuanzia shule ya chekechea had kidato cha nne ni ya lazima. Tangu hapo hata hivyo, jamii zimekuwa zikiwanyima wanawakiwa wengi elimu. Kwamba kunao wachache wanaowaelimisha baadhi ya wanawakiwa, ni kweli. Hata hivyo, wengi hukosa hata wa kuwapeleka katika shule ya chekechea, hivyo kuishia kutojua hata kuandika majina yao. Mfikirie mtu katika karne ya 21, asiyejua kusoma wala kuandika! Nani ajuaye, huenda huyo mwanamkiwa asiyepelekwa shuleni ndiye angalikuwa profesa, daktari, mwalimu, rubani au msomi mtajika na mtaalamu wa uwanja muhimu katika jamii!

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Kila mtoto ana haki ya kulelewa hadi kufikia utu uzima kabla ya kupewa majukumu mazito. Katika katiba ya Kenya, utu uzima, ulio umri wa kuanza kufanya kazi huanzia miaka 18. Wanaohakikisha watoto hawa wametimiza utu uzima kabla ya kufanyishwa gange ngumu wanafaa pongezi. Hata hivyo wanawakiwa wamekuwa wakitumiwa na wengi kama punda wa huduma. Wanaaila wengine huwachukua wanawakiwa kwa machozi mengi wazazi wao waagapo nakuapa kuwahifadhi na kuwatunza wana wale wa ndugu zao, kumbe ni machozi ya simba kumlilia swara! Hata kabla ya mwili wa mzazi mhusika kuliwa na viwavi, mateso kwa mtoto yule huanza, akawa ndiye afanyaye kazi zote ngumu. Utakuta watoto wao wamekaa kama sultan bin jerehe huku mwanamkiwa yule akiwapikia, kuwafulia nguo, kudeki, karibu hata awaoshe miili! Kazi kama zile za shokoa huwa za sulubu na aghalabu husindikizwa kwa matusi yasiyoandikika.

Baadhi ya waja walionyimwa huruma huwahadaa wanawakiwa na kuwapeleka ng'ambo wakitumia vyambo, kuwa wakifika kule watapata kazi za kifahari. Maskini wale hushia kushikwa shokoa, wakawa watumwa katika nyumba za waajiri wao, bila namna ya kujinasua. Wengine hushia kutumiwa kama watumwa wa 'kimapenzi' katika madanguro, miili yao ikawa ya kuuziwa makahaba waroho wasiojali utu. Kujinasua kule huwa sawa na kujitahidi kuokoa ukuni uliokwishageuka jivu, maadamu wanawakiwa aghalabu hukosa watu wenye mioyo ya huruma ya kuwashughulikia. Wengi huitumia methali 'mwana wa ndugu kirugu mjukuu mwanangwa' kuwapuuzilia mbali wanawakiwa ambao hukimbiliwa tu wabinafsi hawa wanapofaidika wenyewe.

Maswali

a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. **(alm1)**

b) Eleza dhana ya mwanamkiwa kwa mujibu wa kifungu. **(alm2)**

c) Eleza imani za kijadi kuhusiana na wanawakiwa. **(alm2)**

d) Jadili masaibu yanayowakumba wanawakiwa. **(alm4)**

e) Eleza haki mbili za kikatiba zilizokiukwa kuhusiana na wanawakiwa. **(alm4)**

f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na kifungu. **(alm2)**

i) Inakera

ii) Majukumu

2. UFUPISHO (Alama 15)

Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelea kutetemesha usalama wa wananchi. Hivi ni vitendo vya kinyama vinavovyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa. Inaghadhabisha kuona Wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuawa kinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kuamba kuwa magaidi hawa wamelaaniwa na siku zao zimehesabiwa hapa duniani. Damu ya mwananchi asiye na makosa katu watailipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini; vita hivi si

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na imani ya kumuua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, Wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi, mauaji, unajisi, ubakaji na maovu mengine. Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila mbinu kuhakikisha kuwa haki za kikatiba za Wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yao zimedumishwa. Lakini cha kusikitisha ni kuwa, mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa ile ya kufanya misako inayoishia kuwanasa mamia ya raia wasio na habari kuhusu kinachoendelea, inawaongezea Wakenya mateso. Hali hii inawaacha kwenye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.

Matumizi ya mbinu hii ya misako yameishia kunasa raia wengi wasio na makosa.Wanaponaswa, hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadha na hata kama wanaaachiliwa huwa tayari wameteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika, mbinu hii inaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani, magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati, polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina yao na majasusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

Maswali

(a) Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu suala la ugaidi (alama 7,1 utiririko) (maneno 60-70)

(b) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50 fupisha aya mbili za mwisho. **(alm 6, 1 utiririko)**

3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a. Tofautisha kati ya sauti /m/ na sauti /b/ . **(alm1)**

b. Unda neno lenye muundo huu: Irabu+ Irabu+ Irabu **(alm1)**

c. Weka kiimbo kwenye sentensi hii ili kuibua maana tatu. Musa amefariki **(alm3)**

d. Weka maneno haya kwenye ngeli mwafaka. **(alm2)**

i. Maiti _____

ii. Kipofu _____

e. Eleza maana ya neno mofimu. **(alm 1)**

f. Tunga neno lenye viambishi vifuatavyo: **(alm2)**

i. Kiima nafsi ya pili umoja

ii. Hali timilifu

iii. Mtendwa

iv. Mzizi

v. Kauli ya kutendea

vi. Kiishio

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

g. Tambua aina za maneno kwenye sentensi hii. **(alm 2)**

Baba yangu alienda kanisani. _____

h. Changanua sentensi hii kwa matawi. Mtoto mdogo analia sana. **(alm 3)**

i. Tambua aina za vishazi kwenye sentensi hii. Utapita mtihani ukisoma kwa bidii. **(alm2)**

j. Andika katika hali ya udogo wingi. Kiti cha mvulana huyu kimepotea. **(alm2)**

k. Kwa kutolea mifano, onyesha matumizi **mawili** ya ritifaa. **(alm2)**

l. Tambua Kipozi, kitondo na ala katika sentensi. Okwero alimpikia Gitau chakula kwa sufuria. **(alm3)**

m. Tambua aina mbili za virai kwenye sentensi hii. Kiatu change kiliraruka baada ya kushonwa. **(alm2)**

n. Nyambua vitenzi hivi kwenye kauli zilizowekwa mabanoni. **(alm3)**

i. Kimbia (tendesha) _

ii. Choma (tendua) _

iii. Ficha (tendama) __

o. Unda nomino kutokana na kitenzi **Pika** . **(alma1)**

p. Andika kinyume cha sentensi hii. Tajiri aliyebarikiwa ni huyu. **(alm1)**

q. Tolea maana za misemo hii**.** **(alm 2)**

i. Vaa miwani

ii. Enda mbweu

r. Tunga sentensi zenye vivumishi vinavyoleta dhana hizi: **(alm3)**

i. Kumiliki

ii. Bila kuchagua

iii. Kuonyesha mbali sana

s. Andika kwenye usemi wa taarifa. (alama 3)

" Unaitwa nani?" Mwalimu alimuuliza. " Naitwa Mahat. " Akajibu.

t. Tunga sentensi moja kuonyesha Kitenzi kishirikishi kipungufu. **(alm1)**

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

1. Jadili changamoto zozote tano zinazoikumba lugha ya Kiswahili. **(alm10)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM THREE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI PP2 KARATASI NAMBARI: 05

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Kwa kipindi cha miezi kadha iliyopita tumeshuhudia vyombo vya dola vikitia makali yake kwenye upekuzi na hata kupiga doria usiku na mchana katika jitihada za kulinda nchi.

Mpango huu ni kweli umeonekana kufanya kazi hivi kwamba hata magaidi wenyewe wameshindwa kupenya katika miji na sasa kuhiari kijinga kushambulia magari ya abiria, kitendo ambacho ni cha kuonyesha uwoga. Kwa hatua hiyo, navipa vyombo vya dola kongole. Jambo ambalo lafaa kujulikana ni kwamba mikakati ya kulinda nchi haifai kuwa ni ya wakati mmoja tu, mbali inafaa kuwa ni zoezi la kila siku.

Magaidi nao huwa macho huku yakijua bayana kwamba wakati wa kulala kwa walinzi unapokuwepo, basi wanapata nafasi ya kututupia 'viazi' ukipenda grunedi.

Kama ilivyo kawaida katika mataifa mengi barani Afrika, ni bayana kwamba bado kungali na mianya mingi ambayo magaidi wa kimataifa huendelea kutumia. Dosari bado zipo. Kwa mfano, mipaka mingi ya nchi hizi huwa kama lango kuu la ugaidi wa kimataifa, kwani kuenea kwa saratani ya ufisadi halimo tu maofisini mbali pia kwenye mipaka yetu.

Kama kupata kitambulisho, pasipoti na stakabadhi zingine za kusafiri nchini Kenya ashakum si matusi ziligeuzwa 'maandazi' ya Kariakoo basi niambie ni nani hawezi kuingia na kutoka nchini bila usumbufu wowote ule bora tu anayehitaji ana hela mkononi? Kwa kuikubali hongo kuwa ufunguo wa kila kitu, Wakenya wenzangu hapo naona ni kama tumejiweka kwenye kikaango kilicho juu ya moto mkali. Hapa hakuna aliye na bahati, tajiri kwa masikini wamo kwenye mtego huu hatari.

Kwa mtindo ambao tunafuata wa kutoa ajira katika idara mbalimbali za ulinzi, inabidi serikali iwe na uangalifu sana hasa kwenye suala nzima la kuhakikisha stakabadhi wanazohitaji si ghushi.

Pasina kufanya hivyo hapo tena tunaweza kuwapata maadui wanaopenya na kujifanya walinzi wetu kumbe ni majasusi wa magaidi. Kila Mkenya anafaa kujihisi kulindwa. Miji, vijiji na hata vitongoji vinafaa kuwa na usalama wa kutosha, kwani kila Mkenya ni mlipa ushuru na hatufai kuona labda tabaka la juu likipendelewa huku mitaa ya mabanda ikiachiwa mbwa koko kama walinzi wao.

Suala lingine muhimu ni kuangaziwa upya usalama kwenye magari ya usafiri.

Juzi tulishuhudia mabasi mawili yakilipuliwa kwenye barabara ya Thika huku tukijua fika kwamba, mpango wa walinda nchi ungalipo.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

La kusikitisha ni kuona kwamba, madereva na utingo wao walikamatwa na kufunguliwa mashtaka kwa kutozuia shambulizo hilo. Je, hii ni sheria gani? Dereva ataendesha gari au atachukua jukumu la walinda usalama?

Waswahili walinena kwamba ukubwa ni jaa na kwa hivyo Rais wa taifa ndiye anayefaa kubeba mzigo mzima wa usalama wetu bila kubananga wasaa. Wengine ambao wanafaa kuwajibika ni wakuu wote wa idara mbalimbali za usalama.

Usalama wako na wangu ni muhimu, elewa bayana kwamba bila usalama watalii hawawezi kuja kututembelea. Bila ya usalama maendeleo ya taifa kamwe hayawezi kupatikana, ndiposa kila jitihada sharti zifanywe ili wote waweze kuendelea kuyafurahia matunda ya uhuru wetu.

Ada ya mja kunena muungwana ni vitendo, hatufai tu kuimba wimbo wa 'linda nchi' ilhali mabasi barabarani hayana usalama. Hebu na tuuone ulinzi endelevu na hapo tutawakomoa magaidi kwa yakini.

Maswali

1. Ipe taarifa hii anwani mwafaka. **(alm1)**

2. Kwa nini magaidi wanashambulia magari ya abiria? **(alm1)**

3. Kulingana na taarifa pamoja na maoni yako, eleza njia tatu ambazo zinatumiwa na magaidi ili kufanikisha utekelezaji wa unyama wao. **(alm3)**

4. Ni njia gani ambazo magaidi hutumia kuingia katika nchi wanapoazimia kutekeleza uhalifu? **(alm3)**

5. Kwa nini suala la usalama kwenye magari ya usafiri muhimu? **(alm1)**

6. Ni njia zipi zinazoweza kutumiwa kupunguza mashambulizi ya kigaidi kulingana na mwandishi? **(alm2)**

7. Eleza athari za utovu wa usalama. **(alm2)**

8. Eleza neno au mafungu ya maneno kama yalivyotumiwa katika kifungu. **(alm2)**

a) Vyombo vya dola

b) Jaa

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Ponografia ni tendo, maandishi, picha au mchoro unaoonyesha au kueleza uchi wa mtu au vitendo vya ngono kwa ajili ya kuchochea ashiki ya kuifanya. Mambo haya machafu huwasilishwa ana kwa ana kupitia sinema, video, magazeti, vitabu, muziki, televisheni. DVD, n.k.

Ponorafia imekuwepo tangu jadi, hasa katika nchi za magharibi. Lakini sasa limekuwa tatizo sugu. Hii ni kwa sababu imeenea ulimwenguni kote mithili ya moto katika mbuga wakati wa kiangazi.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Uenezi umechangiwa na mambo kadha wa kadha. Mchango mkubwa zaidi umetokana na kuimarika kwa vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano. Matumizi ya tarakilishi, mdahilishi na viungambali vya picha yamesambaza ponografia ilivyoanza. Hata hivyo, hubuniwa au kutengenezwa na makundi mbali mbali ya watu. Miongoni mwa hawa ni watu wasiojali maadili. Pili, kuna wale wenye matatizo ya kisaikolojia na kijamii. Wao hutengeneza na kueneza uchafu huu kwa lengo la ama kuvuruga maadili katika jamii au kuchukiza wanajamii waadilifu. Kundi lingine ni lile la wanaoichukulia ponografia kama nyenzo ya kutosheleza ashiki zao. Hivi sasa, kundi kubwa ni lile la wanotumia matusi haya kama njia ya kuchuma. Kwa mfano, wanamziki ambao hutumia ponografia kuvutia wateja na hivyo kuzidisha mauzo yao.

Kushamiri kwa wimbi na uonyeshaji ponografia kuna athari kubwa kwa jamii na hasa watoto. Ingawa watu wengine hudai picha hizi haziwaathiri, upo ushahidi kuonyesha kuwa wanaotazama picha za ngono hupata matatizo. Lazima ieleweke kuwa kinachoonekana na jicho au kusikika kwa sikio huathiri fikira au hisia. Picha za matusi zinachangia kwa kiasi kikubwa kuharibu akili. Badala ya kuzingatia mambo muhimu kama masomo watu huanza kutafakari mambo machafu.

Vijana wengi ni kama bendera. Hivyo basi huanza kuiga wanayoyaona na kusikia. Hili ni tatizo linalowafanya kuacha mkondo wa maadili. Kutokana na uchafu huu, watu wengi hushawishiwa kuingilia shughuli za ngono mapema kabla hawajakomaa kimwili, kiakili na kihisia. Matokeo yake ni mengi. Haya ni pamoja na ukahaba, utendaji mbaya shuleni, mahudhurio mabaya darasani na mimba zisizotarajiwa. Vijana wengi huacha shule kabisa. Wengine nao huambukizwa magonjwa ya zinaa ambayo huwaletea mauti.

Inasemekana kuwa akili za binadamu hunata zaidi mambo yanayowasilishwa kwa picha. Si ajabu vijana huyadumisha matusi haya katika kumbukumbu zao na kuyasanya sehemu ya maisha yao. Wengi huanza kuandama tabia mbovu kama ushoga, ubasha na usagaji. Kuna wale ambao huanza kujichua. Kujichua ni hali ya mwanamke au mwanaume kumaliza haja za kimaumbile bila kufanya mapenzi na mtu mwingine. Ponografia imechangia pakubwa kuenea kwa haya.

Jambo hili limegeuza mielekeo ya vijana. Wanaiga mitindo mibaya ya mavazi yanayoanika uchi wao. Hali kadhalika, huiga lugha, ishara na miondoko inayohusiana na ngono. Yote haya yanapingana na desturi za Mwafrika. Si ajabu visa vya ubakaji vinaongezeka kila kukuchapo.

Utazamaji wa picha chafu aghalabu huandamana na maovu mengine kama unywaji pombe, matumizi ya dawa za kulevya, uvutaji sigara na utumiaji wa dawa za kuchochea uchu wa ngono. Mambo haya huwapa vijana kutazama tabia za unyama.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Jambo hatari ni kuwa kuendelea kutazama picha hizi huzifanya nishai na hisia za watu kuwa butu, yaani huondoa makali. Hata katika utu uzima, mtu atapoteza mhemko wa kawaida na kugeuzwa kuwa mtegemezi wa ponografia. Tatizo hili linaenea kwa vishindo mijini na vijijini. Ipo haja ya dharura kuikinga jamii kutokana na maenezi haya yasio na kizuizi.

Jambo la kwanza ni kuongeza ufahamu wa umma wote kuhusu uovu wa picha hizi. Kwa namna hii itawezekana kupunguza mahitaji na uuzaji wa ponografia. Tatizo hili linaenea kwa vishindo mijini na vijijini. Ipo haja ya dharura kuikinga jamii kutokana na maenezi haya yasiyo na kizuizi. Tatizo la kuenea kwu ponografia limeendelea kuwepo kwa sababu ya udhaifu wa sheria. Kilichoko basi ni kuweka sheria za kuzuia utengenezaji wa upujufu huu. Kuambatana na haya, hatua kali zichukuliwe kwa wanaovunja sheria hizi. Hali kadhalika, ushirikiano wa karibu baina ya wadau uimarishwe katika ulimwengu mzima. Serikali na wanaohusika wakabiliwe ipasavyo. Jamii ingependa kuona michakato ya kuharamisha utengenezaji, usambazaji na utangazaji wa ponografia ikiwekwa.

Wazazi nao wasijipweteke tu bali nao wasaidie. Ni muhimu washikilie kwa sharti juhudi zao za kuwaelekeza na kuwashauri watoto kuzingatia uongofu na kukwepa picha hizi najisi. Watoto lazima waeleweshwe kuwa haifai kutazama picha au michoro michafu. Itikadi na imani za kidini na utamaduni wa Kiafrika unakataza vikali mtu kuona uchi wa mtu mwingine. Matokeo ya kuasi makatazo haya yana madhara makubwa kwa watu na jamii.

Maswali

a) Fupisha ujumbe wa aya ya pili na ya tatu kwa maneno 20 – 25 (ala 6, 1 ya mtiririko)

b) Kwa kutumia maneno 55 – 60, eleza mambo muhimu yanayojitokeza katika aya ya nne hadi ya tisa kuhusu athari za ponografia . (ala 9, 1 ya mtiririko)

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

1. Andika sifa bainifu za /**d**/ na /**f**/. **(alm2)**

2. Andika kinyume cha sentensi hii. **(alm2)**
Mama alianika nguo zilizofuliwa na Kitwana.

3. Andika neno ‘kuja’ katika hali ya kuamuru. **(alm1)**

4. Weka shadda katika neno ‘nta’. **(alm1)**

5. Yakinisha sentensi ifuatayo. **(alm2)**
Wanafunzi wasipopita mtihani huo mwalimu hatalaumiwa.

6. Kwa kutolea mifano, eleza miundo mitatu ya silabi za Kiswahili. **(alm3)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

7. Andika kwa udogo. **(alm2)**

Chaka la Samba halilali paka.

8. Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali. **(ala4)**

Kiongozi aliyeng'olewa mamlakani amekufa.

9. Mzizi ni nini? Toa mfano. **(alm2)**

10. Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mstari. **(alm2)**

Mjadala huo mzuri uliisha usiku wa manane.

11. Tofautisha sentensi hizi: **(alm2)**

a) Ningeondoka sasa ningefika mapema.

b) Ningaliondoka sasa ningalifika mapema.

12. Toa maana mbili za sentensi hii. **(alm2)**

Aliletewa ng'ombe na mtoto wake.

13. Tunga sentensi moja kubainisha. **(alm2)**

Kivumishi cha pekee cha kusisitiza.

14. Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano. **(alm2)**

a) la (fanyia)

b) suka (tendata)

15. Fafanua aina ya hali zilizotumika katika sentensi hizi. **(alm3)**

a) Mumo akacheka, akafurahia na akalala.

b) Mtoto wa Maria hulia kila mara.

c) Mwalimu aandika ubaoni.

16. Tumia neno 'karibu' katika sentensi kama: (**alm2)**

a) Kihusishi

b) Kihisishi

17. Tenganisha mofimu katika neno lifuatalo kisha uonyeshe majukumu yake kisarufi. **(alm3)**

Onana

18. Bainisha yambwa katika sentensi hii. **(alm2)**

Simu aliyonunuliwa Ali na mjombake imepotea.

19. Tumia kivumishi kionyeshi cha mbali pamoja na nomino katika ngeli ya I–I. **(alm1)**

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

a) Eleza wajibu wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa nchini Kenya. **(alm5)**

b) Fafanua sifa za sajili ya matanga. **(alm 5)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM THREE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI PP2 KARATASI NAMBARI: 06

SEHEMU A.UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kisha kisha ujibu maswali:-

Waajiri wengi wanazilaumu taasisi za elimu kwa kukosa kutoa wafanya kazi wenye ujuzi tosha, hasa wa kiteknolojia za kisasa kama kutumia kompyuta kutenda kazi mbalimbali. Hali hii imekuwa ya kuhuzunisha sana.

Ujuzi wa kuweza kutumia Kompyuta unaweza kumfaa mwanafunzi hata anapokosa nafasi ya kujiunga na chuo kikuu kwa vile anaweza kuendelea na elimu yake kupitia kwa elimu mtandao. Pia anaweza kufanya utafiti wa kina kupitia intaneti na kwa njia hii akaimarisha elimu yake.

Mojawapo ya njia ya kuimarisha elimu kuhusu maswala ya teknolojia ni kuanzishwa kwa mikakati mipya ya kufunza. Somo la Kompyuta laweza kuimarika mashuleni endapo kwanza walimu watahamasishwa juu ya faida za ujuzi huu.

Kwa kutumia Kompyuta kufunza, walimu wanaweza kufunza madarasa kadhaa katika kipindi kimoja bila kulazimika kuyahudhuria. Hii itapunguza kiwango cha kazi kwa walimu kwa vile watapata muda wa kufanya utafiti mpana. Aidha, watapata habari na ufahamu zaidi wa mambo kwa kutumia mitambo ya Kompyuta kutoka kwenye intaneti, kupitia tovuti.

Hata hivyo mipango hii inakabiliwa na changamoto kama vile bei za juu za mitambo na vifaa vya Kompyuta, ukosefu wa miundo msingi itakayowezesha utumiaji wa mitambo hii na ukosefu wa walimu waliohitimu somo la Kompyuta.

Pia, kuna tatizo la ukosefu wa nguvu za umeme hasa maeneo ya mashambani; vile vile, katika maeneo yaya haya, wanafunzi na wazazi wengi huvichukulia somo la Kompyuta kuwa gumu na linalofaa wakaazi na wanafunzi kutoka maeneo ya mijini na linalofaa wakaazi muhimu kwao mashambani.

Maswali

(a) Ipe taarifa uliyoisoma anwani inayoifaa **AL.2**

(b) "Hali hii imekuwa ya kuhuzunisha." Ni hali gani inayozungumziwa katika aya ya ? **AL.2**

(c) Ujuzi wa kutumia Kompyuta unaweza kumfaidi vipi mwanafunzi? **AL.4**

(d) Mikakati mipya ya kuimarisha elimu kuhusu maswala ya teknolojia inakabiliwa na vizingiti vipi? **AL.3**

(e) Taja manufaa mawili ambayo mwalimu anaweza kupata kutokana na ujuzi wa teknolojia ya Kompyuta **AL.2**

(f) Andika msamiati mwafaka zaidi kwa maneno yafuatayo: AL.2

(i) Kompyuta_____

(ii) Intaneti _____

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

SEHEMU B.UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma taarifa hii kisha ujibu maswali

Umaskini ni tatizo sugu katika jamii. Binadamu wengi hujikuta katika hali hii kwa sababu hawakubahatika kusoma. Baadhi yao huenda walijaribu kusoma wakashindwa mapema kujipandisha kielimu. Ukosaji wa elimu huchangia sana katika kukuza ukata. Elimu huweza mtu kupata tonge kwa kujipatia kazi za kumwezesha kuyakidhi mahitaji ya maisha. Hali kadhalika, elimu humsaidia binadamu kupata maarifa mengi ya kutendea shughuli zake za kimaendeleo. Kwa mfano, kama ni wakulima wanaweza kutumia **pembejeo** zifaazo ili kuboresha uzalishaji wa mazao. Wakulima wenye elimu hawatapendelea njia duni za kuendeleza kilimo kama vile kutumia visagilima na mbinu nyingine za kijadi. Badala yake watatumia njia za kisasa za kuvunia mazao yao.

Umaskini mwingine huwa mwiba wa kujichoma. Baadhi ya watu ni mikunguni. Kulaza damu kwao kunawafanya kuwa wategemezi katika familia na jamii kwa jumla. Kwa vile hawajazoea kuinamia cha mvunguni, hata wakifunzwa kuchakura hawawezi. Ili kujaribu kuutibu uwele wao na ufukara baadhi yao hutafuta njia za mkato kama vile upwekuzi wa vitu vya wale waliojitahidi. Wakifanikiwa huweza **kufurisha vibindo vyao.** Hata hivyo mkono mrefu wa walinda usalama ukiwakumbatia wao hubakia kusagika kwa dhiki isiyomithilika ndani ya magereza.

Majanga ya kimaumbile kama vile mitetemeko ya ardhi, mikurupuko ya maradhi hatari, moto, ukame na mafuriko huchangia na kuzidisha umaskini. Matukio hayo yakiandama kidindia watu wengi huhasirika. Licha ya mali nyingi kupotea, manusura huachwa wakiwa maskini hohehahe. Matumizi yao hupotea kwani wengi huhitajika kuanza maisha upya.

Vijana ni nguzo muhimu katika maendeleo ya nchi yoyote ile. Endapo watajiingiza katika uraibu wa dawa za kulevya, wataathirika wao wenyewe na jamii kwa jumla. Pamoja na kuwa vijana hawa hufuja pesa nyingi katika ununuzi wa dawa hizi, dawa zenyewe huwadhoofisha na kuwapoka nguvu za kushiriki katika uzalishaji mali. Kutokana na hali hii,umaskini hupaliliwa na kushamiri zaidi.

Umaskini huzua matatizo mbalimbali katika jamii. Ufukara huchachawiza juhudi za serikali za kuwapa raia wake mahitaji ya kimsingi kama vile huduma za afya. Pia umaskini husababisha maovu mbalimbali ya kijamii kama vile mauaji na ukahaba.

Baadhi ya wanajamii huona kwamba njia ya kipekee ya kukabiliana na changamoto zinazosababishwa na hali ya ulitima ni kupitia kwa biashara haramu. Hali hii huchochea zaidi kudorora kwa maadili ya kijamii.

Mataifa mbalimbali ulimwenguni yamezua mikakati mahsusi ya kukabiliana na umaskini. Baadhi ya mataifa yamebuni utaratibu maalum wa kupunguza mwanya mkubwa uliopo kati ya matajiri na maskini. Mojawapo ya mipango hiyo ni kupandisha viwango vya kodi inayotozwa wenye mishahara minono na wafanyibiashara wenye pato kubwa. Aidha huduma za burudani hutozwa

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

kodi ya kiwango cha juu. Kupitia kwa kodi hizo, na njia nyinginezo, serikali za nchi hizo hupata pesa za kuwahudumia maskini.

Mataifa yanayoendelea yanaweza kuwakwamua wananchi kiuchumi kwa kuwapa wahitaji mitaji ya kuanzisha miradi mbalimbali ya kimaendeleo. Mifano ya miradi hiyo ni viwanda vya 'Jua kali', ususi wa vikapu na uchongaji wa vinyago. Hali kadhalika, serikali inaweza kuwatafutia masoko ya nje wafanyi biashara wadogo wadogo. Aidha, serikali inaweza kupunguza ushuru kwa bidhaa zinazoagizwa na masoko ya nje wafanyibiashara wa aina hiyo. Mathalan, ushuru unaotozwa nguo kuukuu zinazoingizwa nchini ukipunguzwa, wauzaji wa nguo hizi watafaidika zaidi na hali ya umaskini itaendelea kupungua.

Sehemu za mashambani ni mhimili mkubwa wa uchumi. Ingawa kumekuwa na juhudi za kuzistawisha sehemu hizi kwa kusambaza huduma za umeme na maji kwa gharama nafuu, bado hali haijawa ya kuridhirisha. Ili kuimarisha sehemu hizi na kukabiliana vilivyo na tatizo la umaskini, hatuna budi kusambaza huduma hizi hasa katika sehemu kame. Sehemu hizi zikipata maji, kilimo chenye natija kitaendelezwa na umaskini utakuwa karibu kuzikwa katika kaburi la sahau. Ikiwa tutazitekeleza sehemu hizi, vijana wanaoweza kusistawisha watahamia mjini kutafuta maisha 'bora'. Hali hii itazidisha msongomano wa watu mjini.

Umaskini ni nduli ambaye lazima aangamizwe ima fa ima. Vijana hawana budi kubadili mtazamo wao hasa kuhusu kazi za mashambani na kujitahidi kuimarisha kilimo. Fauka ya hayo, mifumo mwafaka ya elimu ibuniwe ili kukidhi mahitaji ya kiuchumi ya taifa. Badala ya kuhimiza elimu ya kinadharia, elimu tekelezi isisitizwe zaidi ili wale wanaokosa kazi za kiafisi waweze kujiajiri katika kazi za kiufundi. Ukusanyaji wa ushuru uimarishwe zaidi. Hali ya usalama iendelee kustawishwa ili kuzidi kuwavutia wawekezaji, na hivyo kubuni nafasi zaidi za kazi.

Maswali

(a) Kulingana na kifungu '**umasikini ni hali inayoletwa na udhaifu wa mtu binafsi**'. Jadili (maneno 30-40) **AL.7**

(b) Jamii ina uwezo wa kukabiliana na hali ya umaskini inayowakumba raia wake. Thibitisha kwa mujibu wa kifungu (maneno 40-50) **AL.8**

SEHEMU C.MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40)

(a) Eleza sifa za sauti /ch/ **(alm2)**

(b) Badilisha sentensi ifuatayo iwe mazoea kwa kutumia kirejeshi "O". **(alm2)**

Mtoto anayelia huchapwa

(c) Pambanua viungo vya kisarufi katika neno lifuatalo. **(alm3)**

Tuliwalimia

(d) Tunga sentensi ukitumia neno mzee kama: **(alm2)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

(i) Kivumishi

(ii) kielezi

(e) Jaza mapengo. **(alm3)**

Kutenda	Kutendewa
Pa	_____
Cha	_____
Nya	_____

(f) Eleza maana ya misemo ifuatayo. **(alm2)**

(i) Giza la ukata

(ii) Meza mate machungu

(g) Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo. **(alm3)**

Maksundi alimjengea Tamari nyumba kwa matofali mazuri.

(h) NSomino zifuatazo zinapatikana katika ngeli gani? **(alm2)**

(i) Topasi _____

(ii) Kambare ___

(i) Andika sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo. **(alm2)**

Mizizi ya mibaruti hii iliwaponya watu ambao walikuwa na shida kama hii yenu (kanusha kwa umoja).

(j) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia kielelezo matawi. **(alm4)**

Mwizi aliyetuibia jana amekamatwa hatimaye.

(k) Tunga sentensi yenye masharti yafuatayo. **(alm 3)**

(i) Kiima

(ii) kiarifu

(iii) chagizo

(l) Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa huku ukikanusha. **(alm3)**

Kijibwa chake ni kikali

(m) Jaza neno ambalo ni kinyume cha lile lililopigwa mstari katika sentensi. **(alm2)**

(i) Vile vitu <u>ulivyovichanganya</u> itakubidi

(ii) Bomba hili <u>limeziba</u> mwite fundi aweze

(n) Andika katika usemi halisi. **(alm3)**

Mama aliwahimiza warudi siku hiyo la sivyo wangekosa tuzo.

(o) Tambulisha kishazi tegemezi na kishazi huru. **(alm2)**

Wanafunzi waliofanya vyema walituzwa jana

(p) Kamilisha methali ifuatayo. **(alm2)**

Jitihada za mja____

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

SEHEMU D.ISIMU JAMII (ALAMA 10)

A : Ingia 46! Adams mbao Kenyatta, railways beba! 46 Adams mbao kenyatta, railways!
B: Namba nane ngapi?
A: Mbao ingia, blue.
B: Nina hashuu.
A: Blue Auntie.
B: Sina.
A: Ingia. 46 Adams mbao, kenyatta railways gari bebabeba.
C: Mimi sinako shirini. Chukuako tu kumi.
A: Dinga inakunywanga petrol mzee.
C : Kumi mingi.
A : Haaya ingia twende. Driver imeshona twende.

Maswali

(i) Eleza muktadha wa mazungumzo haya **AL.2**

(ii) Taja sifa **nane** za lugha inayotumika katika sajili hii **AL.8**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM THREE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI PP2 KARATASI NAMBARI: 07

SEHEMU YA A: UFAHAMU(ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

"Asubuhi moja ilinipata ndani ya afisi ya mwalimu mkuu wa Shule ya Kilimo. Mwalimu Mkuu, Bi. Tamasha alisikiliza kadhia yangu kwa makini. Hakuonyeha kushtuka kwa yaliyonipata katika umri wangu mdogo hivi.

'Unaweza kuanza masomo katika darasa la pili. Nitamwomba mzazi mmoja akupe hifadhi,' alisema Bi. Tamasha. Huo ndio uliokuwa mwanzo wa maisha yangu katika makao ya wafanyikazi wa mashamba ya chai. Bwana Tenge na mkewe, Kimai, walinichukua kunilea pamoja na watoto wao watano. Wenzangu, nyinyi hamjui adha zinazowapata wafanyakazi wa kima kidogo. Mtajuaje na haamjawahi kukikalia kitanda hiki mkafahamiana a kunguni wake? Ninayowaambia ni asilimia ndogo mno ya niliyoyaona. Chumba cha wafadhili wangu kilikuwa hichohicho kimoja; ndicho cha mlazi, ndicho cha mpokezi, ndicho jikoni. Sebule na chumba cha malazi viligawanywa na shuka moja nyepesi. Usiku sisi watoto tulilala juu ya vigodoro ambavyo ni kama viliwekwa mvunguni mwa kitanda cha wazazi.

"Usiniulize niliyaona na kuyaskia mangapi katika chumba hiki ambacho kiligeuka *danguro* wakati Bi. Kimai alipokuwa ameenda mashambani. Wakati huu Bwana Tenge angeamua kumleta mwanamke mmoja baada ya mwingine, hapo hapo, mbele ya macho ya wanawe, hadi usiku wa kuamkia siku ya kurudi kwa Bi. Kimai. Mara mojamoja Bi. Kimai angerudi bila kutarajiwa na kumshika ugoni mke mwenzake!Mwaa mmoja, miwili, mitatu ... hata nikaona kwamba, mbali na dhiki za kisaikolojia nilizozipata kwa kushuhudia vituko vya kila aina, nilikuwa mzigo mkubwa kwa wahisani wangu. Si kwamba waja hawa walinibagua, la! Kusema hivyo kutakuwa kuwapaka mashizi bure. Hata hivyo nilihisi kwamba nimepata mbavu za kufanya angaa kibarua kidogo, na kuwatua wawili hawa mzigo wa kuninunulia sare na madaftari.

"Nlianza kuchuna majani chai kwa malipo kidogo nikiwa katika darasa la tano. Wakati mwingine ningerauka alfajiri na mapema kufanya kazi kabla ya kwenda shuleni saa kumi na mbili asubuhi. Jioni nilipitia huko huko. Nyakati nyingi nililala humo humo katikati ya michai, wakati mwingine kwa marafiki wanfu, kwa Bwana Tenge, na juu ya uchaga mkubwa wa saruji uliotumiwa kama karo na wauza chakula sokoni. Hakuna mmoja kati ya walimu wangu aliyejua mabadiliko haya hadi pale nilipoufanya mtihani wangu wa darasa la nane na kufuzu vyema.

"Wakati huo Bwana Tenge alikuwa ameishi kupewa uhamisho, akaenda kufanya kazi katika shamba lingine. Ndivyo wafanywavyo wafanyakazi hawa; kuhamishwa kila uchao bila mtu

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

kuwazia kwamba wana watoto wanaoenda shule, na kwamba kuhamahama huku kunawavurugia masomo wana hawa.”

Maswali

i) Eleza namna wazazi wanavyoweza kuchangia katika kuzorotesha maadili ya watoto katika jamii. **(al.2)**

ii) Onyesha namna haki za watoto zilivyokiukwa katika kifungu. **(al.3)**

iii) Wafanyakazi wa kima kidogo hupitia dhiki zipi kulingana na kifungu? **(al.3)**

iv) Eleza sifa tatu za mkewe Tenge – Kimai. **(al.3)**

v) Eleza namna ndoa inavyosawiriwa katika kifungu. **(al.2)**

vi) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu; **(al.2)**

a. Danguro

b. Kisaikolojia

SEHEMU YA B (ALAMA 15)

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali

Ripoti za kila mara kuhusu uharibifu wa pesa za umma katika serikali za kaunti ni za kusikitisha. Kuna mabilioni ya pesa za mlipa ushuru ambazo hufujwa katika serikali kuu, na hivyo basi wananchi wanakosewa sana wanapoona mtindo huu ukiendelea pia katika serikali za kaunti. Wakati katiba ilipopitishwa mwaka wa 2010, wakenya wengi walikuwa na matumaini mno kwamba ugatuzi ungewatatulia matatizo ambayo walikuwa wakipata katika tawala zilizotangulia, hasa katika maeneo yaliyotengwa kimaendeleo.

Miaka tisa baadaye, kuna mafanikio ambayo yamepatikana ila hatua kubwa zaidi inaweza kupigwa katika kuboresha maisha ya raia kama mianya inayotumiwa kufuja pesa za umma itazibwa. Wizi huu unaojumuisha pia jinsi magavana wanavyobuni nafasi za kazi zisizo na maana ambazo wakati mwingi hupeanwa kwa jamaa na marafiki wao, ni sharti ukomeshwe mara moja. Kuna wananchi wengi ambao tayari wameanza kufa moyo kuhusu umuhimu wa ugatuzi ilhali ukweli ni kwamba hatungependa kurejelea utawala ulio chini ya serikali kuu pekee. Changamoto za ugatuzi zinazosababishwa na ulafi wa viongozi wachache zinatoa nafasi kwa wakosoaji wa mfumo huu wa uongozi kushawishi wananchi na hata wahisani wasishughulike kuchangia kaatika maendeleo ya kaunti zao.

Juhudi zozote zile za maendeleo haziwezi kufanikisha bila ushirikiano kutoka kwa wananchi na wahisani na hivyo basi ni jukumu la viongozi kuonyesha nia ya kutumia mamlaka waliyopewa kwa manufaa ya raia. Tume ya maadili ya kupambana na ufisadi (EACC) kufikia sasa imeonekana kufanya kazi nzuri kwa kuwasaka na kuwashtaki magavana walio mamlakani na wengine walioondoka, kwa kushukiwa kufuja mali za umma. Tungependa asasi zote

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

zinazohusika na masuala ya kupambana na uhalifu, pamoja na wadau wengine katika jamii wenye nia njema kwa wananchi wasifumbie macho maovu yanayotendwa katika kaunti zetu. Nchi hii inatawalwa kwa misingi ya kisheria na hivyo basi hakuna sababu kumhurumia kiongozi yeyote anayekiuka sheria anapokuwa mamlakani kwa msingi wa mamlaka aliyoshikilia. Ni kupitia adhabu kali za kisheria pekee ambapo tutafanikiwa kukomesha uongozi mbaya kwani kama wananchi watakuwa wakisubiri kuwaadhibu wahusika kwa kuwaondoa mamlakani pekee, watakuwa wametoa nafasi ya ufujaji kwa viongopzi wapya kila miaka mitano.

Maswali

a. Fupisha ujumbe wa aya tatu za kwanza kwa maneno 80. (al.8, 1 ya mtiririko)

b. Fupisha aya mbili za mwisho kwa maneno 70. (al.7, 1 ya mtiririko)

SEHEMU YA C (ALAMA 40)

a. i) Elezea sifa mbili za sauti /e/. **(al.1)**

ii) Elezea maana ya sauti mwambatano. **(al.1)**

iii) Onyesha mfano mmoja wa sauti mwambatano. **(al.1)**

b. i) Elezea maana ya kiimbo. **(al.1)**

ii) Elezea umuhimu wake. **(al.2)**

c. Onyesha miundo miwili tofauti ya nomino zipatikanazo katika ngeli ya U-ZI. **(Al.1)**

d. Bainisha mazingira mawili ambapo alama ya kiulizi (?) hutumika. **(al.1)**

e. Bainisha aina mbili za silabi katika neno; Alhamisi. **(al.2)**

f. Yakinisha katika wingi. **(al.1)**

Mwalimu hakumwadhibu mwanafunzi.

g. Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali timilifu. **(al.1)**

Mtoto analala

h. Onyesha aina mbili za mofimu katika sentensi ifuatayo. **(al.2)**

Mimi ninasoma vizuri

i. Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. **(al.3)**

RN+RT+RN

j. Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale. **(al.3)**

Mbaywayu na korongo ni ndege ambao huishi.

k. Bainisha aina za shamirisho. **(al.3)**

Mwalimu alimwandikia mwanafunzi maagizo kwa kalamu.

l. Bainisha aina ya vishazi katika sentensi. **(al.2)**

Mwanafunzi aliyekuwa akisoma amechoka.

m. Andika visawe vya maneno haya. (al.2)

i. Heshima – **ii.** Ruhusa -

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

n. Eleza maana mbili ya fungu hili. **(al.2)**

Jua lile

o. Onyesha matumizi ya kiambishi 'ku' katika sentensi ifuatayo. **(al.2)**

Opiyo atakutengenezea mpini wa jembe na kukuletea kwako.

p. Andika sentensi hii upya ukitumia vinyume vya maneno yaliyopigiwa mstari. **(al.2)**

Mwanafunzi aliketi kisha akakitega kitendawili.

q. Tunga sentensi moja moja ukitumia vitenzi hivi kwa kauli uliyopewa. **(al.2)**

i. La – (tendeana)

ii. Vaa - (tendwa)

r. Andika kwa msemo wa taarifa. **(al.2)**

"Tusipofanya kazi yetu kwa bidii na kujitegemea, tutabaki kuwa watumwa katika nchi yetu," Rais alisema.

s. Tumia 'O' rejeshi kama kiwakilishi. **(al.1)**

Msichana ambaye huja shuleni mwetu ni mwanasheria.

t. Bainisha aina ya virai vilivyopigiwa mstari. **(al.2)**

Mhadhara huo tata ulitolewa jana jioni.

SEHEMU YA D (ALAMA 10)

a) Taja lahaja zozote nne katika kiswahili. **(al.4)**

b) Elezea nadharia zozote tatu ambazo huelezea chanzo cha kiswahili. **(al.3)**

c) Fafanua sifa zozote tatu za salamu katika mazungumzo. Toa sababu tatu. (**al.3)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM THREE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI PP2 KARATASI NAMBARI: 08

1. **UFAHAMU** (Alama 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali

Nilianza kusikia habari za ugoniwa wa ukimwi mnamo mwaka wa 1984. Wakati huo nilikuwa nimemaliza masomo yangu ya kidato cha sita na kujiunga ia chuo cha walimu kilichoko wilayani Nyeri kiitwacho Kagumo. Nilihofu sana maradhi hayo hasa nilipowaona walioambukizwa wakikondeana mthili ya ng'onda. Baada ya waathiriwa kufariki, jamaa zao hawakuruhusiwa kuwazika. Wizara ya afya ilitoa amri kali kuwa wale wore waliofariki kutokana na maradhi ya ukimwi wazikwe na kikundi maalum cha madaktari ma wauguzi wa hospitali za wilayani. Kulikuwa na kasisi mmoja tuliyehusiana kiukoo aliyefariki kutokana na maradhi ya ukimwi. Sisi hatukuruhusiwa hata kumsongea karibu marehemu alipoletwa nyumbani.

Madaktari na wauguzi walivalia majoho meupe ungedhani ni malaika. Mikononi walivaa glovu nyeupe ambazo zilitutisha machoni.

Mara nyingi nimeshangazwa na athari za ugonjwa huu. Inasemekana kuwa kuna njia kadha za usambazaji wa ugonjwa wa ukimwi. Njia moja ni kuhusika katika kitendo cha mapenzi na mtu ambaye ameambukizwa virusi vya ugonjwa huo. Njia nyingine nimeelezwa kuwa ni kwa kutumia kwa pamoja vifaa vyenye makali na mtu aliyeambukizwa virusi vya ukimwi. Inasemekana kuwa kugusa damu ya mtu aliyeambukizwa ugonjwa huo pia kunaweza kukutia mashakani.

Mama mja mzito aliyeambukizwa ugonjwa huu anaweza kumwambukiza mtoto aliye tumboni anapojifungua na hati baadaye anapomnyonyesha mtoto wake mchanga. Kisha kuna kupokea damu kutoka kwa mtu ambaye tayari ameambukizwa virusi hivyo. Yote hayo yanachangia pakubwa katika kututumbukiza kwenye janga hili la ukimwi.

Lakini nimewahi kusikia watu wakisema kuwa ukimwi si maradhi. Yaani ni upungufu tu wa kinga ya kukabiliana na magoniwa katika mwili wa binadamu. Maadamu ukiweza kuimarisha kinga ya magonjwa katika mwili wako basi unaweza kuishi kwa miaka ma mikaka. Anachohitajika mtu ni apate chakula na lishe bora, afanye mazoezi ya kutosha, na kujiepusha na mahusiano ya kimapenzi na watu wenine ambao huenda wakamwambukiza aina tofauti tofauti za virusi vya ukimwi. Hayo yakifanyika mwathiriwa huwa na matumaini ya kuishi kwa muda mrefu kwani hatazidiwa na maradhi hayo na mwishowe kwenda jongomeo. Kuna haja kubwa ya kujilinda na kuepukana kabisa na janga hili lililotuzingira. Wengi tayari wameshapoteza roho zao. Wengine walioambukizwa wanaugua mahospitalini ma na majumbani mwao kisirisiri. Mungu atujalie heri

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

na shari, kwani utafiti wote ambao umefanywa kuhusu tiba ya uwele huu haujafua dafu hata kidogo. Hata hivyo Mola hamtupi mja wake.

Maswali

a) Ipe habari hii anwani ifaayo. **(alm1)**

b) Kwa nini mwandishi ana hofu sana ya maradhi ya ukimwi? **(alm2)**

c) Hapo awali watu waliwachukulia vipi walioambukizwa maradhi ya Ukimwi? **(al2)**

d) Eleza njia mbalimbali zinazomfanya mtu kuambukizwa maradhi ya ukimwi. **(al3**)

e) Je, tunawezaje kuepukana na janga hili la ukimwi? **(alm2)**

f**)** Eleza maana ya vifungu hivi vya maneno kama vilivyotumika katika taarifa. (**alm5)**

i) Wauguzi

ii) Makali

iii) Virusi

iv) Uwele

v) Janga

MUHTASARI

Soma kifungu kifuatacho kwa makini kisha jibu maswali.

Sayansi ya lugha kwa mujibu wa matumizi yake katika jamii ni taaluma mpya sana katika silabasi ya somo la Kiswahili kwa shule za Sekondari. Taaluma hii mpya imeibuka na kuibua hali ya taharuki si kwa wanafunzi, si kwa walimu na si kwa washikadau wote wa kitengo maalum cha kukuza lugha nchini.

Wanapoulizwa sababu ya taharuki yao, jibu huwa ni moja, “Kuku mgeni hakosi kamba mguuni”Jambo la kimsingi ni kuwa mahuluki hutumia lugha katika shughuli ainati.Aidha ni dhahiri shahiri kwamba katika shughuli hizi kuna matumizi ya lugha — ama maneno kwa sauti au ishara kama zile za vipofu na viziwi.

Lugha itumiwapo katika shughuli au taaluma fulani mahsusi, huwa pana msamiati fulani wa kipekee unaotawala katika shughuli hiyo. Istilahi hizi ndizo huunda sajili. Mathalani, katika taaluma ya zaraa kuna istilahi kama vile kulima, kupalilia, kuchimba makoongo, kuandaa weu, kupiga matuta, miche, mbegu, mbolea, jembe, koleo, mundu, mifugo, mazao na istilahi nyinginezo.

Msamiati kama huu ndio huunda istilahi za sajili ya zaraa.

Mbali na zaraa, kuna sajili nyingine kama sajili ya matangazo ya mpira utibabu, mazungumzo ya watoto wa mitaani; biashara, sheria na mahakama, dini ya Kikristo, Kiislamu na ya Kihindu na sajili nyinginezo.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Waama, bila lugha matendo yote ya wanadamu yangegonga mwamba na kudorora. Je, viongozi wangetawala vipi? Wafanya biashara wangenadi vipi bidhaa zao? Walimu wangefunzaje'? Bila shaka jibu ni moja tu: ingekuwa vigumu sana.

Hivyo basi lugha ni chombo muhimu sana. Katika maisha ya waja. Shime kila mtu, tuendeleze lugha yetu ya Kiswahili. Tusiwe *wendaguu* kwani makofi hayalii ila kwa viganja viwili.

a) Fupisha aya tatu za mwanzo kwa maneno yasiyozidi 60. **(Alm7)**
b) Fupisha aya tatu za mwisho kwa maneno yasiyozidi 40. **(alm8)**

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) Toa sita bainifu za sauti /h/ **(alm2)**
b) Tumia neno "hadi" kama kihusishi cha **(al.2)**
(i) Wakati (**ii)** Mahali
c) Onyesha matumizi mawili ya parandesi katika sentensi **(alm2)**
d) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi tofauti ya
(i) – ki –
(ii) – po - **(alm2)**
e) Unda nomino ukitumia mizizi ifuatayo; **(alm2)**
(i) – f –
(ii) – l –
f) Kanusha
Sisi ndisi wakulima **(alm2)**
g) Andika kwa msemo wa tarifa
Askari: Ulikuwa unaelekea wapi uliposhambuliwa?
Jirani: nilikuwa nikienda sokoni jana. **(alm2)**
h)(i) Eleza dhana ya shamirisho **(alm1)**
(ii) Onyesha aina tofauti za shamirisho katika sentensi hii. **(alm2)**
Ali alimnunulia Asha viatu kwa pesa zake
i) Andika sentensi ifuatayo kwa udogo / wingi **(alm2)**
Mtoto mkaidi aliiba kitabu cha mwenzake.
j) Bainisha virai katika sentensi ifuatayo **(alm3)**
mtoto wake aliketi kando ya barabara asubuhi sana
k) i) Nini maana ya kiima? **(alm2)**
ii) Onyesha kiima katika sentensi ifuatayo **(alm2)**
watoto walisafiria basi

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

l) Changanua sentensi kwa kutumia jedwali **(alm4)**

Wachezaji vikapu watakaofanikiwa katika mechi hiyo watatuzwa medali.

m) Tunga sentensi yenye muundo wa:-

kiima, kiarifu, yambwa tendwa, yambwa tendewa na yambwa ala **(alm2)**

n) Bainisha matumizi ya "ni" katika sentensi zifuatazo. **(alm2)**

(i) Ondokeni

(ii) Kiptoo ni mwinzi sugu.

o) Huku ukitoa mifano, eleza maana ya silabi funge **(alm2)**

p) Yakinisha katika nafsi ya tatu wingi **(alm2)**

Sijasafiri kwenda Marekani **(alm 2)**

4. ISIMU JAMII (alama 10)

a) Eleza sababu zozote **sita** zinazochangia kufa kwa lugha **(alm6)**

b) Taja mambo yoyote **manne** yanayofanywa na serikali yetu kuimarisha lugha ya Kiswahili **(alm4)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM THREE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI PP2 KARATASI NAMBARI: 09

1. UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Ilikuwa jumamosi. Nilifika nyumbani kwangu saa moja jioni. Tangu nistaafu miaka miwili awali sikupenda kuchelewa Taarifa ya habari.

Mwezi mmoja ukawa umepita tangu nipewe pesa za kiinua mgongo. Mwezi mmoja mzima nilikuwa katika shughuli za kulipa deni hapa na kulipa karo huku. Kuwekeza kwenye mradi ule na kununua hili. Sasa shilingi lake mbili tu zilikuwa zimesalia katika benki. Watu wengi walinishawishi nijaribu kilimo cha mahindi. Bei ilikuwa imeanza kuimarika. Katika taarifa ya habari jioni hiyo, Waziri wa Kilimo alitangaza bei mpya. Shilingi 1,500 kwa kila gunia. name nilikuwa naanza kuumakimikia mradi huu.

Baada ya tarifa, nilikoga, nikala na nikaenda kulala. Kwa sababu ya uchovu, usingizi ulinichulua mara moha. Usingizi niliota. Katika ndoto niliutekeleza mradi wangu. Msimu huo wa kilimo nilitenga ekari kumu za shamba langu. Wataalamu walinishauri kuwa wakati mzuri wa kulima ni wa kiangazi. Mwezi wa Januari ulipoanza tu nilitafuta trekta na kulima. Malipo yalikuwa shilingi 1,200 kila ekari. Katikati ya mwezi wa Machi, nilitafuta trekta la kutifua shamba tena kwa gharama ya shilingi 15,000 ekari zote kumi. Kufuatia ushauri wa manyakanga wa kilimo, nilipa shilling elfu kumi na tatu kupiga shamba lote haro.

Mwishoni mwa mwezi huo, nilienda mjini kutafuta pembejeo. Kwanza, nililipa shilling 20,500 kwa magunia 15 ya mbolea. Kisha nilinunu amagunia manne ya mbegu ya mahindi yenye uzani wa kilo 25 kwa shilling 3,300 kila gunia. Mwzi wa Aprili ulipotimia tu, niliamua kupanda. Ili nipate mazao bora, nilipanda kwa tandazi. Gharama ilikuwa shilling 1,000 kila ekari. Mvua ilinesha vizuri na baada ya siku saba mahindi yalianza kuota. Ilifurahisha kuhesabu mistari ya kijani iliyonyooka. Hali hii iliwezekana tu baada ya kuajiri vijana wa kuwafukuza korongo na vidiri ili wasifukue mebgu mchangani.

Baada ya mwezi mmoja, hatua ya kupalilia ilifika. Nilitafuta vibarua wa kupalilia. Malipo yalikuwa shilingi 700 kila ekari. Kumbe kupalilal kulichochea mtifuko wa mahindi. Punde yakawa yananifikia magotini. Hii ikawa ishara kuwa yanahitaji kumwagiwa mbolea ya kunawirisha iitwayo ‘amonia’. Gharama yake ikawa shilling 1,300 kila gunia. Hivyo, nikalipa shilingi 19,500 kwa magunia kumi na matano.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Mahindi yalibadilika kimiujiza. Ghafla tu yalirefuka na kunenepa maisha. Yalibadilika rangi yakapiga weusi. Shamba liligeuka likawa kama msitu wa rangi ya kijani iliyokolea. Wapita njia waliajabia mimea na juhudi zangu. Shamba langu sasa likawa kielelezo. Maafisa wa kilimo wakawa kila siwanawaleta wakulima wengine kujifunza siri ya ufanzi wanfu. Hapo nikaanza kuhesabu mavuno nitakayopata kukadiria faida. Nilipuuza kabisa ushauri wa wahenga kuwa 'Usikate majani, mnyama hajauawa.'

Bila taarifa wala tahadhari mvua ikatoweka. Hayakupita majuma mawili mahinda yakaanza kubadilika. Juma moja baadaye mahindi yalinyauka. Badala ya mahind, shamba ilkageuka la vitunguu vilivyochomwa na jua. Makasio yangu ya faida yaliyeyuka jinsi yfanyavyo moshi.
Lakini 'Muumba ndiye Muumbua'. Siku moja mawingu yalitanda na mvua ikanyesha.Muda si muda mahind yalianaza kunawiri. Kumbe tukio lililonivunja moyo lilikuwa laja. Siku moja mvua kubwa ilinyesha. Asubuhi nilipotoka nje nilipigwa na butwaa. Barafu ilitapakaa pote. Shamba lilikuwa limetapakaa barafu huku majani ya mahindi yamechanika kama nyuzi. Niliugua. Baada ya wiki moja, nilipata nafuu. Nilipotazama upande wa shamba nikaona dalili za majani mapya ya mahindi yakianza kuchomoza. Maumbile ni kitu cha ajabu kweli. Muda sio mferu mahindi yalirudi hali yake tena, kisha yakakomaa. Haraka za kutafuta watu wa kuyakata na kuyakusanya zilianza. Gharama ya shughuli kii ikawa shilingi 5,000. Kuvuna, kusafirisha kutoka shamba na kukoboa kwa mashine magunia 200 yakachukua shilingi 20,500. Kufikia hapo nilikuwa nimetumia takribani shilingi 192,700. Gharama nyingine zilikuwa za usafiri, gharama ya dharura na usimamizi, usumbufu wangu binafsi, gharama ya magunia na kadhalika. Mahindi yalipokuwa tayari kwenye magunia nilifunga safari kwenda mjini kutafuta soko. Niliposhuka tu niliona gazeti. habari motomoto siku hiyo ilikuwa: "MAHIND GUNIA 900/-" Niligutuka usingizini.

Maswali

(a) Andika kichwa mwafaka kwa kifungu hiki cha habari. **(al 1)**

(b) Msimulizi alikuwa na kiasi gani cha pesa katika benki baada ya mradi kukamilika? **(al 1)**

(c) Taja matatizo matatu yaliyotisha mradi wa msimulizi wa kukuza mahindi. **(al 3)**

(d) Eleza maana ya methali zifuatazo: **(al 4)**

(i) Usikate majani, mnyama hajauawa

(ii) Muumba ndiye muumbua

(e) Eleza mambo mawili yaliyosababisha msimulizi asipate faida alivyotarajia. **(al 2)**

(f) Kwa nini msimulizi alisem maumbile ni kitu cha ajabu? **(al 2)**

(g) Eleza maana ya: **(al 2)**

(i) kiinua mgongo

(ii) manyakanga wa kilimo

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

2 UFUPISHO (alama 15)

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwauchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea uwezo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema ‘maarifa ni nguvu.’

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti,kuyaendesha, kuyatawalana kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanawezakuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: ‘Elimu ni mali.’ Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu huweza kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishswa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano,kitabu.

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambabmba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana kwa mfano, neno ‘mwerevu’ huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa ‘mjinga’, ‘ mjanja’, ‘hodari’ na kadhalika.

Maarifa huweza kunifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu,ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Maarifa hayawezi kuthibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapomfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe,ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za uenezaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

(a) Fupisha aya ya pili na tatu (maneno 55-60)(alama 5, 1 ya utiririko)

(b) Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane.
(maneno 100-110) (alama 10, 2 za utiririko)

Matumizi ya lugha (alama 40)

a. Taja na utofautishe irabu za mbele. **(alm2)**

b. Tunga sentensi Moja kubainisha maana mbili za neno kikosi. **(alm2)**

c. Andika katika wingi. **(alm1)**
Jino langu bovu linaloniuma linanitatiza.

d. Tumia kielezi cha wakati badala ya kielezi kilichotumika katika sentensi ifuatayo. **(alm2)**
Watalii walitutembelea mjini Nakuru.

e. Geuza sentensi zifuatazo kulingana na maagizo. **(alm2)**
i. Maimuna anapika wali. (wakati uliopo hali isiyodhihirika)
ii. Wao walisoma riwaya hiyo. (wakati ujao hali timilifu)

f. Unda neno lenye muundo ufuatao. **(alm2)**
i. Nafsi ya kwanza umoja.
ii. Hali timilifu
iii. Mtendewa
iv. Mzizi
v. Kauli ya kutendea
vi. Kauli ya kutenda/ kiishio

g. Tumia nomino zifuatazo za kawaida kuunda nomino za jamii. **(alm2)**
i. Nzige **ii.** Zabibu

h. Tunga sentensi kuonyesha matumizi yafuatayo ya neno KAMA. **(alm2)**
i.Kihusishi
ii.Kitenzi

i. Eleza matumizi ya neno <u>wale</u> katika sentensi hii. **(alm3)**
Wale walioiba ni mabanati wale ambao waliambiwa wale kabla ya kitendo hicho.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

j. Changanua kwa mstari. **(alm4)**

Yohana na Otieno hucheza kandanda.

k. Andika sifa tatu zinazobainisha sentensi changamano. **(alm3)**

l. Onyesha matumizi ya viwakifishi vifuatavyo katika sentensi. **(alm2)**

i. Kibainshi

ii. Parandesi

m. Tumia neno –baya kama: **(alm3)**

i. Kiwakilishi

ii. Kivumishi

iii. Kielezi katika sentensi

n. Onyesha miundo miwili ya nomino za ngeli ya A- WA. **(alm2)**

o. Bainisha maana mbili ya sentensi hii. **(alm2)**

Umu alimwandisha mkewe.

p. Unda nomino nne kutokana na kitenzi. **(alm4)**

Fa

q. Geuza katika usemi halisi. **(alm2)**

Askari jela alimuuliza Kendi kama alidhnani hapo ni kwao.

Alimwamuru aende kwake mara moja.

4. **ISIMU JAMII** **(alama 10)**

(Mdundo wa muziki) kina mama mpo…..! Kina siste nanyi… are you there? Kampuni ya platinium imewaletea mafuta mpya ya silk. Mafuta hayo yana vitamin C, Sunscreen na yana marashi ya kupendeza. Ukiyatumia kwa wiki moja tu, ngozi yako itakua laini na nyororo kama ya kitoto kichanga. Nayo macho ya wote, Waaa! Yatakuwa kwako 24/7. Jinunulie! Jinunulie! Mafuta ya silk. Mafuta ya wanawake wa kisasa.

a. Taja sajili iliyotumiwa hapa. **(alm1)**

b. Taja sifa nne za sajili hii. **(alm4)**

c. Kwa nini Wakenya wengi hupenda kuchanganya na kubadili msimbo? **(alm5)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM THREE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI PP2 KARATASI NAMBARI: 10

1. UFAHAMU (alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na uathirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu, msingi mkuu wa uinishaji wa mahusiano hayo ni kukichunguza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano baina ya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache, na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitikadi kuwa uhusiani uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hivyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiani huu hautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu; tutaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi, kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi, na kudumisha uhusiano wetu wa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au kipindi kirefu, unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofubatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili, mahusiano ya kiwango cha wastani, kuna mahusiano yanayohusisha marafaki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mwahali mwa kazi, washirika kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekana kudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya, hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfano wa jamii. Kwa mfano, kwa majirani wanaoishi kwenye janibu, fulami mahususi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri. Uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilikabadilika. Isitoshe, kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kuumomonyoa ukuta wa uhusiano wa kudumu.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano kati ya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wa majirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasa huweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujiri katika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa dukani, kwenye sehemu za ibada, kwenye kituo cha mafuta, kwa kinyozi,kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mapito. Kwanza, uwezekano wa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na "uhusiano wa chembe". Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachomshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, kiatu anachokushonea, nguo anazokufulia, ususi anaokufanyia n.k. mahusiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisiasa na kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzake kwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakula, amefutwa kazi, amefiliwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni: Je, tunahusiana vipi na jamaa zetu, taasisi zetu, marafiki zetu na majirani zetu? Je, uhusiano wetu na raia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

Maswali

(a) Taja kigezo muhimu cha kuzungumzia mahusiano. **(alm1)**

(b) Eleza imani ya watu kuhusu uhusiano baina ya jamaa. (**alm1)**

(c) Fafanua athari ya teknolojia kwenye mahusiano ya watu. **(alm2)**

(d) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo **(alm4)**

(e) Taja sifa kuu ya mahusiano ya muda mfupi. **(alm2)**

(f) Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? **(alm 2)**

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. **(alm3)**

(i) inasigana **(ii)** yameghoshi **(iii)**vighairi

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Ujambazi wa kimataifa ni tatizo ililowasumbua walimwengu kwa muda mrefu sana. Serikali nyingi zimetumia mapesa mengi kwa miaka mingi sana zikijitahidi kupambana na janga hili. Hata hivyo, fanaka haijapatikana, wala halielekei kamwe kuwa itapatikana leo au karne nyingi baadaye.

Yumkini tatizo kubwa lilipo ni kuhusu jelezi la dhana ya "ujambazi" tena "kimataifa". Hili ni tatizo mojawapo na yapo mengi sana. Tatizo la pili ni kiburi. Kuna wale watu binafsi na hasa viongozi wa nchi kubwakubwa na serikali zao zilizojiaminisha kuwa ujambazi ni balaa kweli, tena belua, lakini huo ni wa huko, wala hauwezi kuwagusa licha ya kuwashtua wao.

Kulingana na maoni ya watakaburi hao, ujambazi ni wa watu "washenzi" wasiostaaraka, wapatikanao katika nchi zisizoendelea bado. Ujambazi peke wanaouona unafaa kukabiliwa ni dhidi ya mbubujiko wa dawa za kulevya uliosababishwa na vinyangarika kutoka nci hizo maaluni za "ulimwengu wa tatu". Kulingana na wastaarabu wa nchi zilizoendelea, vinyangarila hivi ndivyo hasa adui mkubwa wa ustaarabu ulimwenguni na ni sharti vifagiliwe mbali bila huruma. Baada ya kusagwasagwa, ulimwengu mstaarabu utazidi kutokana na ahadi ya mbingu hapa ardhini itakamilika.

Imani ya watu hawa ya kuwaa ujambazi wa kimataifa, hata iwapo upo, hauwezi kuwashtua wala kuwatingisha wao ilikuwa kamili na timamu. Ilikuwa kamili na timamu hadi hapo mwezi Septemba tarehe 11 mwaka wa 2001, ndege tatu za abiria zilipolekezwa katika majumba mawili ya fahari, yenye urefu wa zaidi ya ghorofa mia moja na kuyatwangilia mbali. Mshtuko na kimako! Kimako kwa kuwa, kabla ya siku hiyo. Wamarekani hawangeweza kudhani kwamba ingewezekana taifa lolote au mtu yeyote kuthubutu kushambulia nchi yao, taifa wasifa lililojihami barabara dhidi ya ina yoyote ile ya uchokozi kutoka pembe yoyote ya dunia.

Hakuna ulimwenguni mzima, aliyeamini kuwa Marekani ingeweza kushambuliwa. Kwa ajili hiyo, mshtuko uliitingisha ardhi yote na huzuni ilitanda kote, kama kwamba sayari nzima imeshambuliwa, wala sio Marekani pekee.

Mintarafu hiyo, Marekani ilipolipiza kisasi kwa kuwaunguza waliokuweko na wasiokuwemo kwa mabomu hatari huko Afghanistan, idadi kubwa ya watu duniani ilishangilia na kusherehekea. Kwa bahati mbaya, tafsiri ya shambulizi la minara-pacha na Newyork na lile la Pentagon, uti wa uwezo wa kivita wa Marekani, ulizorota. Kuna wengi waliodhani huo ni mwanzo wa vita vya Waislamu dhidi ya Wakristo na kwa muda, Waislamu wote wakashukiwa kimakosa kuwa ni majambazi wa kimataifa.

Maswali

(a) Bila kubadilisha maana, fupisha aya tatu za kwanza. (maneno 60-75) **(alm8)**

(b) Ukizingatia aya tatu za mwisho, fafanua fikira za watu na mambo yote yaliyotokea baada ya Septemba tarehe 11, 2001. (maneno 65 - 75) **(alama 7)**

3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

(a) Toa mfano mmoja wa: **(alm2)**

(i) Kipasuo

(ii) Kitambaza

(b)(i) Kiimbo ni nini? **(alm1)**

(c) Andika maneno yenye miundo ifuatayo ya sauti. **(alm2)**

(i) KIKKKI

(ii) IIIKI

(**d**) Kanusha sentensi ifuatayo: **(alm2)**

Amekuja kukuona na ataondoka kesho

(e) Andika katika usemi wa taarifa. **(alm2)**

"Hicho kijicho cha paka cheupe leo marufuku kwangu". alisema mzee kambumbu

(f) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo **(alm2)**

(i)Chuma

(ii)Zawadi

(**g**) Eleza matumizi mawili ya nukta pacha. **(alm2)**

(h) Andika sentensi ifuatayo katika udogo wingi **(alm2**

Uso wake umefura kabisa baada ya kuumwa na mbwa.

(i) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mchoro wa matawi. **(alm4)**

Mchezaji atakayeshinda atatuzwa zawadi murua

(j) Andika sentensi ifuatayo upya bila kubadilisha maana ukitumia 'O'rejeshi**.** **(alm2)**

Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.

(k) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo: **(alm2)**

Wazee watatu walitoka mangweni mchana.

(L) Onesha kishazi huru na tegemezi

Msichana mtukutu alifukuzwa shuleni leo asubuhi. **(alm2)**

(m) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo mabanoni. (alama 2)

(i) Nata (kutendesha)

(ii) Kaa (kutendana)

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

(n) Bainisha yambwa katika sentensi ifuatayo. **(alm3)**

Mgeni aliandaliwa chakula kitamu na mwenyeji wake kwa sinia.

(o) Tambua matumizi ya kiambishi –ji- **(alm2)**

Jino la jitu hilo lililiwezesha kujilia chakula kingi kuliko mkimbiaji yule.

(p) Tunga sentensi moja kudhihirisha maana ya vitate *rika* na *lika.* **(alm2)**

(**q)** Tambua aina ya vihusishi katika sentensi zifuatazo. **(alm2)**

(i) Jumba lifuatalo li mbele ya msikiti wa Musa.

(ii) Kisiwa cha Giningi kimekauka

(r) Tambua hisia zinazojitokeza katika sentensi hizi: **(alm2)**

(i) Ngo! Mtu kama wewe hawezi kufaulu.

(ii) Maskini! Alikuwa moto maskini.

(s) Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya nahau ifuatayo. **(alm2)**

Zunguka mbuyu

4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)

(a) Eleza dhana ya uwingi lugha. **(alm2)**

(b) Fafanua mambo **manne** yanayochangia uwingi lugha katika jamii. **(alm8)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

CALL AMOBI GROUP OF EXAMINERS @ 0743 333 000 OR 0706 851 439 TO ACQUIRE :









